JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Jengo la Ukaguzi, 16 Barabara ya Samora Machel, S.L.P. 9080, 11101 Dar es Salaam. Simu ya Upepo: 'Ukaguzi' D'Salaam, Simu: 255(022)2115157/8, Nukushi: 255(022)2117527, Barua pepe: ocag@nao.go.tz, Tovuti: www.nao.go.tz

# TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI KUHUSU RIPOTI ZA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNI, 2018

**Prof. Mussa Juma Assad**
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**

8 Aprili, 2019

## YALIYOMO

SURA YA KWANZA ........ 1
UTANGULIZI WA JUMLA ........ 1
SURA YA PILI ........ 3
TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA HATI ZA UKAGUZI ........ 3
SURA YA TATU ........ 7
MATOKEO YA UKAGUZI WA SERIKALI KUU ........ 7
SURA YA NNE ........ 17
MATOKEO YA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA ........ 17
SURA YA TANO ........ 26
MATOKEO YA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA ........ 26
SURA YA SITA ........ 32
MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ........ 32
SURA YA SABA ........ 35
MATOKEO YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO 35
SURA YA NANE ........ 42
MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU ........ 42
SURA YA TISA ........ 47
MATOKEO YA UKAGUZI WA UFANISI ........ 47
HITIMISHO ........ 58

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI WA JUMLA

## 1.1 Utangulizi

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Awali ya yote, ninamshukuru Mwenyezi Mungu aliyetuwezesha kukutana mahali hapa leo. Pia, ninamshukuru Mh. Rais kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha kwake Ripoti za Ukaguzi kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018 na kuwezesha ripoti hizo kuwasilishwa Bungeni kupitia Mawaziri husika kwa mujibu wa Ibara ya 143 (4) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 (ilivyorekebishwa mwaka 2005).

Hii inadhihirisha namna Mh. Rais anavyothamini majukumu ambayo Ofisi yangu imepewa Kikatiba katika kusimamia Rasilimali za Watanzania.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Kwa mujibu wa Vifungu vya 26 hadi 29 vya Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 (kama ilivyorekebishwa), kwa mwaka wa fedha 2017/18 niliweza kufanya kaguzi za aina mbalimbali na hivyo kuwezesha kutoa taarifa zilizowasilishwa bungeni leo tarehe 10 Aprili, 2019 kama ifuatavyo:

1. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu;
2. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa;
3. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Mashirika ya Umma;
4. Ripoti ya Ukaguzi wa Hesabu za Miradi ya Maendeleo;
5. Ripoti ya Ukaguzi wa Mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano;
6. Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi; na
7. Ripoti 11 za Ukaguzi wa Ufanisi katika Sekta mbalimbali na Utekelezaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi kama zilivyoainishwa katika Jedwali Na. 1.

**Jedwali Na. 1: Ripoti za Ufanisi za Kisekta**

| Na. | Ripoti ya Ukaguzi wa Ufanisi kuhusu; | | |
|---|---|---|---|
| 7.1 | Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi wa Miradi ya Umwagiliaji | 7.7 | Ufuatiliaji wa Shughuli za Ujenzi wa Majengo Mijini |
| 7.2 | Usimamizi wa Miradi ya Maji Vijijini | 7.8 | Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya za Rufaa na Dharura kwa Hospitali za Rufaa ngazi ya Juu |
| 7.3 | Usimamizi wa Miradi ya Maji itokanayo na Visima Virefu | 7.9 | Upatikanaji na Usambazaji wa Pembejeo za Kilimo |
| 7.4 | Matengenezo ya Mitambo ya Kuzalisha Umeme | 7.10 | Usimamizi wa Utoaji wa Huduma ya Bima ya Taifa ya Afya Nchini |
| 7.5 | Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalum | 7.11 | Ufuatiliaji wa Mapendekezo ya Ukaguzi wa Ufanisi |
| 7.6 | Usimamizi wa Mfumo wa Ununuzi wa Magari ya Serikali kwa pamoja | | |

# SURA YA PILI

# TATHMINI YA UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO NA HATI ZA UKAGUZI

## 2.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yangu yaliyotolewa miaka iliyopita, pamoja na Hati za Ukaguzi zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2017/18.

## 2.2 Tathmini ya Utekelezaji wa Mapendekezo Yaliyotolewa Miaka Iliyopita

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Katika ukaguzi wangu, nilifanya tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo ya kiukaguzi yaliyotolewa miaka iliyopita na kubaini kuwa Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuyafanyia kazi.

Tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo hayo inaonesha kuwa kati ya mapendekezo 350 yaliyotolewa miaka iliyopita, mapendekezo 80 sawa na asilimia 22.9 yametekelezwa kikamilifu. Mapendekezo 124 sawa na asilimia 35.4, utekelezaji wake unaendelea. Hata hivyo, mapendekezo 72 sawa na asilimia 20.6 utekelezaji wake haujaanza; na mapendekezo 74 sawa na asilimia 21.1 yamepitwa na wakati. Mchanganuo wa utekelezaji umeainishwa katika Jedwali Na. 2.

**Jedwali Na. 2: Hali ya Utekelezaji wa Mapendekezo kwa Miaka Iliyopita**

| Aina ya Ripoti | Idadi ya Mapendekezo | Utekelezaji umekamilika | Utekelezaji unaendelea | Utekelezaji haujaanza | Yamepitwa na wakati |
|---|---|---|---|---|---|
| **Mamlaka za Serikali za Mitaa** | 62 | 4 | 30 | 28 | 0 |
| **Mashirika ya Umma** | 112 | 52 | 36 | 18 | 6 |
| **Serikali Kuu** | 91 | 2 | 17 | 4 | 68 |
| **Ufanisi** | 85 | 22 | 41 | 22 | 0 |
| **Jumla** | **350** | **80** | **124** | **72** | **74** |
| ***Asilimia*** | ***100*** | ***22.9*** | ***35.4*** | ***20.6*** | ***21.1*** |

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Kwa ujumla, utekelezaji wa mapendekezo bado upo chini. Hivyo, ninapendekeza Serikali iongeze jitihada katika kutekeleza mapendekezo yaliyotolewa katika ripoti zangu.

## 2.3 Hati za Ukaguzi Zilizotolewa kwa Mwaka wa Fedha 2017/18

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Katika Ukaguzi wa Hesabu nilioufanya kwa Serikali Kuu na Taasisi zake, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2017/18, nimetoa jumla ya Hati 548 za Ukaguzi. Kati ya hizo, Hati zinazoridhisha ni 531, sawa na asilimia 97; Hati zenye shaka ni 15, sawa na asilimia 2.6; Hati 1 isiyoridhisha, ambayo ni sawa na asilimia 0.2; na Hati mbaya 1, sawa na asilimia 0.2. Jedwali Na. 3 linaonesha mchanganuo wa Hati za Ukaguzi zilizotolewa. Vile vile Jedwali Na. 4 linaonesha Taasisi mbazo zimepata Hati Mbaya na Hati isiyoridhisha

**Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi wa Hesabu kwa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma kwa Mwaka 2017/18**

| Aina ya Ripoti | Jumla ya Hati | Hati Zinazoridhisha | Hati Zenye Shaka | Hati Zisizoridhisha | Hati Mbaya |
|---|---|---|---|---|---|
| Mamlaka za Serikali za Mitaa | 185 | 176 | 7 | 1 | 1 |
| Mashirika ya Umma | 122 | 121 | 1 | 0 | 0 |
| Serikali Kuu | 241 | 234 | 7 | 0 | 0 |
| ***Jumla*** | ***548*** | **531** | ***15*** | ***1*** | ***1*** |
| *Asilimia* | *100* | 97 | 2.6 | 0.2 | 0.2 |

**Jedwali Na. 4: Taasisi zilizopata Hati Mbaya na Hati isiyoridhisha**

| Na. | Taasisi | Aina ya Hati |
|---|---|---|
| **1.** | Halmashauri ya Wilaya ya Nyang'hwale | Hati mbaya |
| **2.** | Manispaa ya Kigoma Ujiji | Hati isiyoridhisha |

Aidha, katika Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokuwa inatekelezwa na Taasisi mbalimbali kwa mwaka wa fedha 2017/18, nimetoa jumla ya Hati za Ukaguzi 469. Kati ya hizi, Hati zinazoridhisha ni 455, sawa na asilimia 97; na Hati zenye shaka ni 14, sawa na asilimia 3.

Vile vile, Katika Ukaguzi wa Vyama vya Siasa kwa mwaka wa fedha 2017/18, nimetoa Hati za Ukaguzi kwa Vyama 14. Kati ya hivyo, Vyama vitatu (3), sawa na asilimia 21 vilipata hati zinazoridhisha; Vyama vinne (4), sawa na asilimia 29 vilipata Hati zenye shaka; Vyama viwili (2), sawa na asilimia 14 vilipata Hati zisizoridhisha; na Vyama vitano (5), sawa na asilimia 36 vilipata Hati mbaya. Jedwali Na. 5 linabainisha Vyama vya Siasa vilivyopata Hati mbaya na Hati zisizoridhisha.

**Jedwali Na. 5: Vyama vya Siasa Vilivyopata Hati Mbaya na Hati Zisizoridhisha**

| Na. | Chama cha Siasa | Aina ya Hati |
|---|---|---|
| **1.** | ADA-TADEA | Hati mbaya |
| **2.** | National Reconstruction Alliance (NRA) | Hati mbaya |
| **3.** | Union for Multiparty Democracy (UMD) | Hati mbaya |

| Na. | Chama cha Siasa | Aina ya Hati |
|---|---|---|
| **4.** | Alliance for Africa Farmers Party | Hati mbaya |
| **5.** | Sauti ya Umma (SAU) | Hati mbaya |
| **6.** | Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMMA) | Hati isiyoridhisha |
| **7.** | National League for Democracy | Hati isiyoridhisha |

## SURA YA TATU

## MATOKEO YA UKAGUZI WA SERIKALI KUU

### 3.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi wa Serikali Kuu. Taasisi na Maeneo yaliyohusika na Ukaguzi ni pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania; Usimamizi wa Deni la Serikali; Udhaifu katika Malipo ya Mafao; na Ukaguzi wa Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Mifuko Maalumu, na Taasisi nyingine. Aidha, Sura hii inatoa mapendekezo kwa Serikali Kuu na Vyama vya Siasa.

### 3.2 Matokeo ya Ukaguzi wa Serikali Kuu

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika Ukaguzi wa Serikali Kuu.

#### 3.2.1 Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

***Usimamizi wa Mapato Yatokanayo na Kodi***

Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikusanya shilingi trilioni 15.38 ikilinganishwa na malengo yaliyowekwa ya kukusanya shilingi trilioni 17.31; hivyo kuwa na nakisi ya makusanyo kwa shilingi trilioni 1.93 ambazo ni sawa na asilimia 11 ya malengo. Jumla ya makusanyo hayo haikujumlisha shilingi bilioni 18.95 ambazo ni Vocha za Misamaha ya Kodi kutoka Hazina. Hivyo, makusanyo halisi ya mwaka 2017/18 ni shilingi trilioni 15.40 yakijumuisha na Vocha za Misamaha ya Kodi kutoka Hazina.

***Kodi Zilizoshikiliwa katika Kesi za Muda Mrefu kwenye Mamlaka za Rufaa za Kodi***

Mamlaka ya Mapato Tanzania ina Mashauri ya Kodi ya Thamani ya shilingi trilioni 382.6 kwenye Mamlaka za Rufaa za Kodi ikiwa ni ongezeko la kiasi cha shilingi trilioni 378.2 (asilimia 8595) ikilinganishwa na shilingi trilioni 4.4 kwa mwaka wa fedha 2016/17. Ongezeko hili limechangiwa kwa kiasi kikubwa na Mashauri manne yenye thamani ya shilingi trilioni 374.7 yanayoihusu Kampuni ya Uchimbaji Madini ya ACACIA.

***Kutokukusanywa kwa Mapato Yatokanayo na Kodi ya Kiasi cha Shilingi Bilioni 46.81 na Dola za Marekani Milioni 2.74***

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Mamlaka ya Mapato Tanzania ilishindwa kukusanya mapato zaidi ya shilingi bilioni 46.81 kutoka kwa walipakodi mbalimbali. Jedwali Na. 6 linabainisha taasisi, aina za kodi, na kiasi cha fedha ambacho hakikukusanywa.

**Jedwali Na. 6: Taasisi ambazo Hazikukusanya Mapato Yatokanayo na Kodi**

| Taasisi | Aina ya Kodi | Kiasi cha Kodi | |
|---|---|---|---|
| | | Shilingi | Dola za Marekani |
| Mamlaka ya Viwanja vya Ndege, Mashirika 19 ya Ndege, na Makampuni ya huduma za Meli | Tozo za huduma za usafiri wa anga na majini | 1,845,250,227.00 | 2,747,249 |
| Makampuni 23 ya Mafuta | Kodi za mafuta | 7,292,580,904.44 | |
| Walipa kodi mbalimbali | Kodi ya bidhaa | 35,223,221,808.42 | |
| Makampuni tisa (9) ya Mafuta | Malipo pungufu ya kodi | 1,167,107,857.00 | |
| Makampuni mbalimbali ya Mafuta | Tozo za huduma za bandari | 1,286,992,434.00 | |
| **Jumla ya Kodi** | | **46,815,153,230.86** | **2,747,249** |

***Udhibiti Usioridhisha wa Bidhaa Zinazopitia Nchini na Zinazosafirishwa Nje ya Nchi***

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Wakati wa uhakiki wa bidhaa zinazoingizwa Nchini na Nchi jirani ili zisafirishwe kwenda Nchi nyingine, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilishindwa kunipatia ushahidi kuthibitisha kuwa kodi ya shilingi bilioni 57.09 ililipwa.

Aidha, nilibaini kuwa bidhaa zilizosafirishwa kutoka Nchini kwenda Nchi nyingine zilizopaswa kutozwa Kodi ya Ongezeko la Thamani ya shilingi milioni 649.45 ziliruhusiwa kwenda nje ya Nchi bila kukamilisha taratibu za Forodha. Mamlaka ya Mapato Tanzania ilishindwa kutoa ushahidi wa nyaraka za kuthibitisha kuwa kodi stahiki zilikusanywa.

### 3.2.2 Usimamizi wa Deni la Serikali

Kufikia tarehe 30 Juni, 2018, Deni la Serikali lilikuwa shilingi trilioni 50.92, ambapo Deni la ndani lilikuwa shilingi trilioni 14.73 na Deni la nje shilingi trilioni 36.19; kiasi hiki ni ongezeko la shilingi trilioni 4.84 sawa na asilimia 10.5 ikilinganishwa na Deni la shilingi trilioni 46.08 lililoripotiwa tarehe 30 Juni, 2017.

Katika ukaguzi wangu, nilibaini masuala ya msingi yafuatayo kuhusu Deni la Serikali na usimamizi wake:

(a) Mapungufu katika usahihi wa taarifa kutokana na udhibiti wa ndani usiojitosheleza katika kuweka kumbukumbu na kutoa taarifa za Deni la Serikali.

(b) Serikali kuchelewa kulipa madeni ya Benki Kuu ya kiasi cha shilingi bilioni 212.7. Kati ya hizo, shilingi bilioni 199.79 zinatokana na riba ya nakisi ya Serikali, na shilingi bilioni 12.9 ikiwa ni sehemu ya Serikali ya gharama za kudhibiti ukwasi kuanzia mwaka 2015/16 hadi 2017/18.

(c) Kutokuwapo kwa uwianishaji wa taarifa za mfumo wa malipo (Epicor) na Mfumo wa Utunzaji wa Taarifa za Deni la Taifa wa Jumuiya ya Madola (Common Wealth Secretariat-Debt Record Management System – (CS-DRMS)). Hii inasababisha taarifa za fedha

kutowiana na vyanzo vyake, hivyo kuhatarisha uadilifu wa taarifa za Deni la Serikali.

### 3.2.3 Udhaifu katika Malipo ya Mafao

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Katika mwaka wa fedha 2017/2018, nilikagua Majalada 2,868, ambapo Majalada 2,814 yenye jumla ya shilingi bilioni 165.44 niliyaidhinisha kwa ajili ya malipo lakini Majalada 54 niliyahoji na kuyarudisha kwa Maofisa Masuuli husika kwa ajili ya masahihisho.

Kati ya Majalada 2,868 yaliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2017/18, Mafao ya Wastaafu 295 (10.5%) yalibainika kukokotolewa kimakosa. Kati ya hayo, Majalada 172 yamebainika kuwa na ziada ya malipo ya shilingi milioni 577.32 huku Majalada 123 yakiwa na upungufu wa malipo wa shilingi milioni 294.35.

Aidha, nilibaini ucheleweshaji mkubwa wa waajiri katika maandalizi na uwasilishaji wa Majalada ya wanufaika wa mafao kwa ajili ya Ukaguzi. Ucheleweshaji huo unatokana na waajiri kutotoa kipaumbele kwenye usimamizi wa uandaaji wa mafao hivyo kuwanyima wastaafu haki yao ya kupata mafao kwa wakati.

### 3.2.4 Ukaguzi wa Wizara, Idara na Wakala wa Serikali, Mifuko maalumu, na Taasisi nyingine

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Nilifanya ukaguzi katika wizara na idara za Serikali 65; wakala za Serikali 33, mifuko maalumu ya fedha 16, na taasisi nyingine za Serikali 42. Nilikagua pia vyama vya siasa 14, balozi za Tanzania 41, bodi za mabonde ya maji 14 na hesabu jumuifu za taifa. Katika ukaguzi wangu, nilibaini mapungufu yafuatayo:

***Udhaifu Uliobainika katika Wakala za Serikali***

(a) Wakala za Serikali hazikupeleka kiasi cha shilingi bilioni 9.26 kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina kama inavyotakiwa na Kifungu cha 11 (3) cha Sheria ya Fedha ya Mwaka 2001 (kama iliyorekebishwa 2016);

(b) Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) unadaiwa kiasi cha shilingi bilioni 57.09 ikiwa ni riba ya ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi wa ujenzi na washauri wa miradi;

(c) Kasi ndogo ya Wakala wa Majengo Tanzania katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa majengo yenye thamani ya shilingi bilioni 24.06. Jedwali Na. 7 linaainisha miradi hiyo

**Jedwali Na. 7: Miradi ya TBA iliyochelewa kukamilika**

| Na. | Maelezo | Kiasi (Sh) |
|---|---|---|
| 1 | Ujenzi wa Jengo la Utawala Halmashauri ya Mji wa Tarime | 3,115,458,992.30 |
| 2 | Ujenzi wa Jengo la Utawala Halmashauri ya Wilaya ya Butiama | 3,265,332,538 |
| 3 | Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Chato kwenye kiwanja Na. 01 Ghorofa A | 9,980,466,628.10 |
| 4 | Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Geita Awamu ya I | 5,972,242,627.12 |
| 5 | Ujenzi wa Nyumba za Viongozi wa Serikali | 724,711,087.80 |
| 6 | Ujenzi wa jengo la Ofisi la Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, Mwanza | 2,499,917,157.57 |
| 7 | Ujenzi wa Nyumba ya Makazi ya Mkuu wa Mkoa kwenye Mkoa wa Mwanza | 660,082,069.23 |
| 8 | Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Awamu ya IV | 397,239,882.38 |
| 9 | Ujenzi wa jengo la ofisi la Halmashauri ya manispa ya Ilemela | 3,833,822,825.42 |
| | **Jumla** | **24,068,482,277.62** |

*(d)* Baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kushindwa kuhamisha fedha zilizokuwa za tozo za wakandarasi na fedha za kodi ya zuio za kazi zenye jumla ya shilingi bilioni 6.65 kwenda Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA).

***Udhaifu katika Utengenezaji wa Vitambulisho vya Taifa Kupitia Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa (NIDA)***

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Katika ukaguzi wa Mamlaka ya Vitambulisho ya Taifa nilibaini kuwa kati ya watu 19,662,105 waliosajiliwa, ni vitambulisho 4,511,809 tu ndivyo vilivyotengenezwa, sawa na asilimia 23 ya idadi ya watu walioandikishwa.

Aidha, nilibaini kuwa Kampuni ya IRIS Corporation Berhad ya Malaysia (Mkandarasi) imesimamisha shughuli zote za kutengeneza vitambulisho kuanzia tarehe 14 Machi 2018. Sababu za kusimamisha zinajumuisha kutolipwa deni la mkandarasi lenye thamani ya Dola za Marekani milioni 30.18 (Shilingi bilioni 69.98), na kutoongezwa kwa muda wa mkataba kwa kipindi cha miezi kumi (10) tangu kwisha kwa muda wa mkataba wa awali, tarehe 14 Machi 2018.

***Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba***

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Katika mapitio ya taratibu za manunuzi na usimamizi wa mikataba kwenye taasisi mbalimbali za Serikali, nilibaini mambo yafuatayo ambayo yanaleta shaka katika kufikia thamani ya fedha.

(a) Kiasi cha shilingi bilioni 4.61 kilitumika kununua bidhaa, huduma, ushauri wa kitaalamu, na kazi za ujenzi ndani ya wizara, idara, na sekretarieti za mikoa pasipo kutumia taratibu za kushindanisha wazabuni kinyume na Kanuni za 163 na 164 za Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013.

(b) Taasisi saba (7) zilifanya manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 5.37 bila kupata vibali vya Bodi za Zabuni kinyume na Kifungu cha 35 (3) cha Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011, na Kanuni 55 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2013. Taasisi hizo ni:

  (i) *Sekretarieti ya Mkoa wa Iringa;*
  *(ii) Sekretarieti ya Mkoa wa Geita;*
  *(iii) Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga;*
  *(iv) Wizara ya Katiba na Sheria;*
  *(v) Jeshi la Polisi;*
  *(vi) Jeshi la Wananchi Tanzania; na*
  *(vii) Ofisi ya Rais - Idara ya Kumbukumbu na Utunzaji wa Taarifa*

(c) Taasisi tano (5) zilifanya manunuzi ya bidhaa, huduma, na kazi za kiasi cha shilingi bilioni 1.17 bila kuwapo kwa makubaliano ya Kimkataba na Wazabuni. Hii ni kinyume na Kanuni Namba 10 (4) ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013. Taasisi hizo ni kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 8

**Jedwali Na. 8: Taasisi zilizofanya manunuzi bila kuwapo na Mikataba na Wazabuni.**

| Na. | Taasisi | Kiasi Sh. |
|---|---|---|
| (i) | Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa | 910,485,775 |
| (ii) | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | 8,920,515 |
| (iii) | Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Maadili ya Watumishi wa Umma | 55,200,000 |
| (iv) | Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro | 9,467,560 |
| (v) | Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto | 190,693,491 |
| **Jumla** | | **1,174,767,341** |

***Udhaifu katika Usimamizi wa Matumizi***

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Katika mapitio ya taarifa za matumizi ya fedha za umma, nilibaini dosari mbalimbali katika udhibiti wa ndani kama ifuatavyo;

(a) Matumizi ya shilingi bilioni 4.66 yalifanywa na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwenda kampuni binafsi za huduma za kisheria bila kufuata makubaliano ya mikataba; na

(b) Taasisi 20 za Serikali Kuu ziliwalipa watoa huduma mbalimbali kiasi cha shilingi bilioni 1.43 pasipo kudai stakabadhi za kielektroniki.

Taasisi hizo ni:

1. Sekretarieti ya Mkoa wa Njombe;
2. Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi;
3. Idara ya Uhamiaji;
4. Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia;
5. Ofisi ya Waziri Mkuu-Ofisi Binafsi;
6. Idara ya Huduma za Magereza;
7. Ofisi ya Waziri Mkuu;

8. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano – Sekta ya Mawasiliano;
9. Sekretarieti ya Mkoa wa Shinyanga;
10. Mahakama ya Tanzania;
11. Sekretarieti ya Mkoa wa Tanga;
12. Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi;
13. Sekretarieti ya Mkoa wa Lindi – Hospitali ya Rufaa Sokoine;
14. Sekretarieti ya Mkoa wa Pwani;
15. Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro;
16. Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;
17. Tume ya Maendeleo ya Usharika Tanzania;
18. Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia,Wazee na Watoto;
19. Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano; na
20. Wizara ya Kilimo;

(c) Malipo yalifanyika kimakosa katika vifungu visivyostahili ya kiasi cha shilingi bilioni 885.99 kinyume na Kanuni ya 42(2) ya Kanuni za Fedha za Umma za Mwaka 2001. Jedwali Na. 9 linaonesha taasisi zilizofanya malipo kimakosa kwenye vifungu visivyostahili.

**Jedwali Na. 9: Malipo Yaliyofanyika Kimakosa kwenye Vifungu Visivyostahili**

| Na | Fungu | Mkaguliwa | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| 1 | 36 | Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi | 25,358,936 |
| 2 | 91 | Mamlaka ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya | 24,975,376 |
| 3 | 92 | Tume ya Kuzuia UKIMWI Tanzania | 13,040,000 |
| 4 | 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | 11,392,600 |
| 5 | 33 | Ofisi ya Rais - Sekretariaeti ya Viongozi wa Umma | 24,756,382 |
| 6 | 2034 | Ubalozi wa Tanzania - Moroni | 430,859,250 |
| 7 | 85 | Sekretarieti ya Mkoa wa Tabora | 4,816,700 |
| 8 | 13 | Kitengo cha Kuzuia Fedha Haramu | 40,210,165 |
| 9 | 48 | Wizara ya Ardhi, Nyumba, na Maendeleo ya Makazi | 27,700,000 |
| 10 | 22 | Deni la Serikali na Huduma za Jumla | 885,391,817,305 |
| **Jumla** | | | **885,994,926,714** |

***Shilingi Bilioni 2.54 za Mapato Yasiyotokana na Kodi ambayo Hayakuwasilishwa Mfuko Mkuu***

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Ukaguzi ulibaini kuwa kiasi cha shilingi bilioni 2.54 kilichokusanywa na Balozi 7 za Tanzania katika mwaka wa fedha 2017/18 hakikuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina kinyume na Kifungu cha 11 cha Sheria ya Usimamizi wa Fedha ya Mwaka 2001. Badala yake, kiasi hicho cha fedha kilibakizwa katika akaunti za fedha za Balozi husika. Jedwali Na. 10 linaonesha makusanyo yaliyofanywa na Balozi, ambayo hayakuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina.

**Jedwali Na. 10:** ***Mapato Yasiyotokana na Kodi ambayo Hayakuwasilishwa Mfuko Mkuu***

| Na. | Kufungu | Jina la Balozi | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|---|
| **1** | 2005 | Ubalozi wa Tanzania Abuja, Naijeria | 295,240,406 |
| **2** | 2001 | Ubalozi wa Tanzania Addis Ababa, Ethiopia | 259,358,949 |
| **3** | 2024 | Ubalozi wa Tanzania Riyadh, Saudi Arabia | 58,580,000 |
| **4** | 2016 | Ubalozi wa Tanzania Stockholm, Swideni | 828,362,785 |
| **5** | 2035 | Ubalozi wa Tanzania, Kuwaiti | 218, 224,308 |
| **6** | 2007 | Ubalozi wa Tanzania Lusaka, Zambia | 93,280,322 |
| **7** | 2018 | Ubalozi wa Tanzania Washington, D.C., Marekani | 784,726,694 |
| **Jumla Kuu** | | | **2,537,773,464** |

***Mapungufu Yaliyobainika katika Ukaguzi wa Vyama vya Siasa***

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyobainika katika ukaguzi wa Vyama vya Siasa.

(a) Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kilinunua gari jipya aina ya Nissan Patrol kwa Dola za Marekani 63,720 (sawa na shilingi milioni 147.76) ambalo lilisajiliwa kwa jina la mwanachama badala ya jina la Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA. Pia, gari hilo

lilioneshwa kwenye taarifa za fedha kama mkopo kwa mwanachama huyo bila kuwa na makubaliano ya mkopo yaliyosainiwa kati ya mwanachama na Bodi ya Wadhamini ya CHADEMA.

(b) Chama Cha Mapinduzi (CCM) hakikuwasilisha michango ya kila mwezi kwenda Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF). Hadi kufikia Mei, 2018 chama hicho kilikuwa na deni la shilingi bilioni 3.74 ambalo linajumuisha adhabu ya shilingi bilioni 2.73 iliyotokana na ucheleweshwaji wa uwasilishaji wa michango hiyo.

(c) Aidha, nilibaini kuwapo kwa tatizo la uendelevu wa biashara (Going concern) katika Kampuni ya Uchapishaji ya Uhuru inayomilikiwa na CCM. Pia, hati za ardhi za nyumba 199 zinazomilikiwa na CCM Zanzibar zilionekana hazijasajiliwa kwa jina la Bodi ya Wadhamini bali zimesajiliwa kwa majina ya maofisa wa Chama.

(d) Vyama saba vilifanya matumizi ya jumla ya shilingi milioni 777.91 bila ya kuwa na nyaraka toshelevu na hivyo nilishindwa kuthibitisha iwapo malipo hayo yalikuwa halali; na iwapo yalihusiana na shughuli za vyama hivyo. Vyama hivyo vimeainishwa katika Jedwali Na. 11

**Jedwali Na. 11: Vyama vilivyofanya Matumizi bila ya kuwa na Nyaraka Toshelevu**

| Na. | Chama | Kiasi (Sh.) |
|---|---|---|
| (i) | Chama cha Ukombozi wa Umma (CHAUMA) | 7,069,000 |
| (ii) | Union for Multiparty Democracy (UMD) | 3,370,000 |
| iii) | Sauti ya Umma (SAU); | 7,404,205 |
| iv) | Alliance for Africa Farmers Party (AAFP) | 9,475,000 |
| v) | Chama cha Kijamii (CCK); | 10,948,800 |
| vi) | Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) | 134,646,740 |
| (vii) | Chama cha Mapinduzi (CCM) | 604,996,994 |
| **Jumla** | | **777,910,739** |

### 3.3 Mapendekezo kwa Serikali Kuu na Vyama vya Siasa

Ili kurekebisha kasoro nilizozibainisha, ninashauri yafuatayo:

(i) Serikali ifanye juhudi za makusudi kuziwezesha Mamlaka za Rufaa za Kodi ili kuhakikisha mashauri ya kodi yanashughulikiwa kwa wakati ili kupunguza mrundikano wa mashauri.

(ii) Serikali idhibiti mifumo ya ukusanyaji wa tozo za huduma za usafiri kwenye viwanja vya ndege na bandari. Pia, Serikali iimaishe udhibiti wa mafuta na bidhaa zinazoingia nchini kwa matumizi ya ndani, na zinazopita kwenda nchi nyingine ili kuhakikisha kuwa zinalipiwa kodi stahiki.

(iii) Serikali iimarishe udhibiti wa ndani katika kuhakiki mikopo iliyopokelewa na taasisi nufaika kabla ya kuingiza kumbukumbu za madeni kwenye mfumo ili kuondoa mapungufu katika usahihi wa taarifa.

(iv) Kupitia Maofisa Masuuli, Serikali iimarishe udhibiti na utaratibu wa kufanya mapitio ya uandaaji wa mafao ili kuhakikisha kuwa kanuni na vigezo vya ukokotoaji na sheria vinazingatiwa ili kuepuka ucheleweshaji wa mafao ya hitimisho la kazi na hasara kwa Serikali.

(v) Serikali itoe kwa wakati fedha za utekelezaji wa miradi ya barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara Tanzania kama ilivyoidhinishwa na bunge ili kuepuka malipo ya ziada yanayotokana na riba.

(vi) Kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali ihamishe mali na madeni yote yanayohusiana na miradi ya barabara kwenda Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini; na Ofisi ya Rais - TAMISEMI inapaswa kufuatilia utekelezaji huo.

(vii) Serikali kupitia Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa iharakishe zoezi la usajili na utengenezaji wa vitambulisho vya Taifa. Pia, itathmini utendaji kazi wa mkandarasi ili kuweza kuamua iwapo imuongezee muda wa mkataba au iingie makubaliano na mkandarasi mwingine.

(viii) Serikali kupitia Taasisi zake iepuke kufanya manunuzi toka chanzo kimoja au kushindanisha vyanzo vichache endapo bidhaa au huduma zinazotakiwa haziendani na zile zilizotajwa katika Kanuni ya 159 ya Kanuni za Manunuzi ya Umma za Mwaka 2013. Hii itasaidia kuwa na usawa na uwazi katika manunuzi ya Umma. Pia, ihakikishe kuwa manunuzi yote yanapata vibali vya Bodi za Zabuni kabla ya kufanyika kwa manunuzi ili kuhakikisha uwepo wa thamani ya fedha katika manunuzi.

(ix) Serikali ihakikishe malipo yote yanafanyika kwa mujibu wa mikataba iliyosainiwa baina ya Taasisi za Serikali na watoa huduma. Vilevile, Taasisi za Serikali zihakikishe zinadai na kupatiwa stakabadhi za kielektroniki pindi zinapowalipa wazabuni ili kuzuia ukwepaji wa kodi.

(x) Uongozi wa Vyama vya Siasa uhakikishe kuwa udhibiti unaanzishwa na kuimarishwa, hasa kwenye malipo, ili malipo yote yawe na vielelezo na nyaraka toshelezi, zikiwamo risiti za kielektroniki.

## SURA YA NNE

### MATOKEO YA UKAGUZI WA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

### 4.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi uliofanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Maeneo yaliyozingatiwa wakati wa ukaguzi ni pamoja na Usimamizi wa Mishahara na Rasilimali-Watu; Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo; Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba; Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma; na Usimamizi wa Makusanyo ya Mapato ya Vyanzo vya Ndani.

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Nimefanya ukaguzi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 185. Katika ukaguzi huo, nimebaini masuala mbalimbali ambayo Serikali inapaswa kuyafanyia kazi ili kuboresha usimamizi wa Rasilimali za Umma katika ngazi ya Serikali za Mitaa. Yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyojitokeza katika ukaguzi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa.

### 4.2 Udhaifu katika Usimamizi wa Mishahara na Rasilimali-watu

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Katika ukaguzi wa mishahara na rasilimali-watu, nilibaini mambo yafuatayo.

(a) Madai mbalimbali ambayo hayajalipwa ya kiasi cha shilingi bilioni 11.1 ambacho ni malimbikizo ya mishahara ya watumishi katika mamlaka za serikali za mitaa 22.

(b) Malipo ya mishahara kwa watumishi waliokoma utumishi wao ya jumla ya shilingi milioni 207.37 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 17. Malipo hayo yanajumuisha shilingi milioni 128.31 kwa Watumishi Waliofariki, Wastaafu, na Watoro/Waliofukuzwa Kazi; shilingi milioni 53.94 ikiwa ni makato ya watumishi hao; na shilingi milioni 25.10 ikiwa ni mishahara iliyolipwa mara mbili katika Halmashauri ya Babati. Jedwali Na. 12 linaainisha Mamlaka za Serikali za Mitaa 17 zilizofanya malipo ya mishahara hiyo.

**Jedwali Na. 12: Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizofanya Malipo ya Mishahara kwa Watumishi waliokoma Utumishi**

| Na. | Taasisi | Mishahara iliyolipwa | Makato | Mishahara mara mbili | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Halmashauri ya Mji wa Babati | 2,048,400.00 | 1,463,600.00 | 25,109,355 | 28,621,355.00 |
| 2. | Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba | 13,585,000.00 | 0 | 0 | 13,585,000.00 |
| 3. | Halmashauri ya Wilaya ya Bumbuli | 5,345,141.00 | 4,414,863.00 | 0 | 9,760,004.00 |
| 4. | Halmashauri ya Mji wa Handeni | 348,948.57 | 656,051.43 | 0 | 1,005,000.00 |
| 5. | Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo | 7,511,436.00 | 6,384,564.00 | 0 | 13,896,000.00 |
| 6. | Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi | 1,485,940 | 1,793,060 | 0 | 3,279,000.00 |
| 7. | Halmashauri ya Mji wa Korogwe | 4,164,779.00 | 4,780,721.00 | 0 | 8,945,500.00 |
| 8. | Halmashauri ya Wilaya ya Kwimba | 4,886,053.00 | 4,397,947.00 | 0 | 9,284,000.00 |
| 9. | Halmashauri ya Wilaya ya Kyela | 21,473,021.00 | 11,996,979.00 | 0 | 33,470,000.00 |
| 10. | Halmashauri ya Wilaya ya Mkinga | 750,251.94 | 1,448,748.06 | 0 | 2,199,000.00 |
| 11. | Halmashauri ya Mji wa Nanyamba | 25,109,571.00 | 0 | 0 | 25,109,571.00 |

| Na. | Taasisi | Mishahara iliyolipwa | Makato | Mishahara mara mbili | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|
| 12. | Halmashauri ya Wilaya ya Ngorongoro | 1,495,515.49 | 700,484.51 | 0 | 2,196,000.00 |
| 13. | Halmashauri ya Wilaya ya Nzega | 0 | 2,937,349.00 | 0 | 2,937,349.00 |
| 14. | Halmashauri ya Wilaya ya Pangani | 685,356.94 | 1,366,643.00 | 0 | 2,051,999.94 |
| 15. | Halmashauri ya Wilaya ya Songwe | 27,566,000.00 | 0 | 0 | 27,566,000.00 |
| 16. | Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru | 2,462,155.95 | 3,894,791.00 | 0 | 6,356,946.95 |
| 17. | Halmashauri ya Wilaya ya Ukerewe | 9,402,252.00 | 7,710,748.00 | 0 | 17,113,000.00 |
| **Jumla** | | **128,319,821.89** | **53,946,549** | **25,109,355** | **207,375,725.89** |

(c) Kiasi cha shilingi bilioni 1.04, ambacho ni makato ya kisheria ambayo hayakuwasilishwa kwa Taasisi husika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 41.

(d) Kiasi cha shilingi milioni 242.66, ambacho ni malipo kwa watumishi wa mikataba bila kuwepo mikataba halisi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa saba (7).

## 4.3 Udhaifu katika Usimamizi wa Miradi ya Maendeleo

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Katika tathmini yangu ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo, nilibaini baadhi ya mapungufu kama ifuatavyo:

(a) Miradi 27 yenye thamani ya shilingi bilioni 5.24 ilikamilika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 16 lakini haitumiki. Jedwali Na. 13 linaainisha baadhi ya miradi hiyo:

**Jedwali Na. 13: Baadhi ya Miradi ya Maendeleo iliyokamilika lakini haitumiki**

| Na. | Mradi uliyotekelezwa | Kiasi cha fedha (Sh.) |
|---|---|---|
| 1 | Nyumba Tano za Watumishi katika kijiji cha Ilungu Halmashauri ya Wilaya ya Magu | 419,109,088 |
| 2 | Ujenzi wa Mochwari, Wodi ya Wazazi, Chumba cha Umeme na Njia za kupita Wagonjwa katika kituo cha Afya Halamashauri ya Wilaya ya Biharamulo | 500,000,000 |
| 3 | Ujenzi wa Mabweni Shule ya Msingi Mahitaji Maalum Kizega Halmashauri ya Wilaya ya Iramba | 221,000,000 |
| 4 | Miradi ya Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara | 1,955,625,406 |
| 5 | Ujenzi wa Madarasa Matano na Choo kimoja katika Shule ya Sekondari Mwandege Halmashauri ya Wilaya ya Mkuranga | 114,570,300 |
| 6 | Majengo ya Hospitali katika Halmashauri ya Wilaya ya Meru | 313,510,000 |
| 7 | Ujenzi wa Jengo la Wagonjwa wa Nje katika Hospitali ya Wilaya Halmashauri ya Jiji la Arusha | 535,518,226 |

| Na. | Mradi uliyotekelezwa | Kiasi cha fedha (Sh.) |
|---|---|---|
| 8 | Ujenzi wa Kituo cha Afya Songwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu | 400,000,000 |

(b) Usimamizi hafifu na kasi ndogo ya utekelekezaji wa miradi umesababisha kutokamilika kwa miradi ya maendeleo yenye thamani ya shilingi bilioni 52.42 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 46.

(c) Kutorejeshwa kwa mikopo iliyotolewa kwa vikundi vya wanawake na vijana katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 90 yenye thamani ya shilingi bilioni 10.04.

## 4.4 Udhaifu katika Manunuzi na Usimamizi wa Mikataba

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Katika ukaguzi wa utekelezaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma, nilibaini mapungufu yafuatavyo:

(a) Manunuzi yenye thamani ya shilingi bilioni 3.93 yalifanyika katika mamlaka 48 za Serikali za Mitaa bila kushindanisha wazabuni.

(b) Manunuzi ya bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi bilioni 9.04 yalifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 32 bila kuidhinishwa na bodi za zabuni.

(c) Bidhaa na huduma zenye thamani ya shilingi milioni 923.83 zilinunuliwa kutoka kwa wazabuni wasioidhinishwa na Wakala wa Manunuzi wa Serikali (GPSA) katika Mamlaka za Serikali za Mitaa18.

(d) Kuondolewa kwa wazabuni wenye bei ya chini bila sababu za msingi na kuisababishia Serikali hasara ya kiasi cha shilingi bilioni 2.36.

(e) Mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 24.85 ilitekelezwa bila kuwepo kwa dhamana ya utendaji.

## 4.5 Udhaifu katika Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma

*Ndugu Waandishi wa Habari*,

Ukaguzi ulibaini udhaifu katika usimamizi wa matumizi ya Fedha za Umma katika baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kama ifuatavyo:

(a) Malipo ya kiasi cha shilingi bilioni 6.71 yalifanyika yakiwa na nyaraka pungufu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 106 hivyo sikuweza kuthibitisha uhalali na ukamilifu wa malipo hayo.

(b) Hati za malipo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.67 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 17 hazikuwasilishwa kwa ajili ya ukaguzi.

(c) Matumizi yasiyostahili ya shilingi milioni 859.14 yalifanyika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 36 kwa sababu hakukuwa na fedha zilizotengwa kwenye bajeti. Kulibainika pia malipo ya aina moja kufanyika mara mbili na malipo ya posho kwa kiwango cha juu zaidi ya kiwango kinachokubalika.

(d) Malipo yasioidhinishwa na wakuu wa idara na Maofisa Masuuli zaidi ya shilingi bilioni 1.03 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 17.

(e) Mamlaka za Serikali za Mitaa 74 zilifanya malipo ya shilingi bilioni 8.5 kwa wakandarasi na watoahuduma mbalimbali bila kudai stakabadhi za kielektroniki.

(f) Mamlaka za Serikali za Mitaa 28 zilifanya malipo ya shilingi bilioni 1.2 bila ushahidi kuwa madai hayo yalikuwa ni sehemu ya madai ya miaka ya nyuma.

## 4.6 Udhaifu katika Usimamizi wa Makusanyo ya Mapato ya Vyanzo vya Ndani

*Ndugu Waandishi wa Habari*,

Katika mapitio ya Sera, Udhibiti wa Ndani, Ufuatiliaji na Mikakati ya kukusanya Mapato iliyoanzishwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, nilibaini mambo yafuatayo:

(a) Mamlaka za Serikali za Mitaa 13 hazikuwa na sheria ndogondogo za kukusanyia mapato kinyume na Kifungu cha 80(1-3) cha Sheria za

Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji) ya Mwaka 1982 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2006). Matokeo yake Mamlaka hizo zinakosa nguvu ya kisheria ya kukadiria au kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali visivyoidhinishwa.

(b) Mamlaka za Serikali za Mitaa 19 hazikukusanya ushuru wa huduma wa asilimia 0.3 ya mauzo ukiondoa kodi ya ongezeko la thamani kutoka katika makampuni 8,613 yanayoendesha shughuli zake katika maeneo ya Mamlaka hizo kinyume na Kifungu Na. 6(1) (u) cha Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya Mwaka 1982 (kama ilivyorekebishwa mwaka 2000).

(c) Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 7, nilibaini kuwapo kwa mashine 56 za kielektroniki za kukusanyia mapato (PoS Machine) ambazo hazikusajiliwa wala kuonekana katika Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS).

(d) Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 8, nilibaini kulikuwa na mawakala 195 wa kukusanya mapato bila kuwepo na makubaliano ya kisheria.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Aidha, niliangalia usimamizi wa mapato na kugundua kuwapo kwa viashiria vya udanganyifu kama ifuatavyo:

(a) Nilibaini makusanyo ya shilingi bilioni 5.26 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 78 hayakuthibitishwa kupelekwa benki kinyume na Agizo la 50(5) la Randama ya Fedha za Mamlaka ya Serikali za Mitaa ya Mwaka 2009.

(b) Marekebisho kadhaa ya ankara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 50 yenye thamani ya shilingi bilioni 9.43 yaliombwa na kuidhinishwa na mtu mmoja katika Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato kinyume na utaratibu wa Udhibiti wa Ndani katika ugawaji wa majukumu.

## 4.7 Mapendekezo

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Ili kurekebisha kasoro na mapungufu yaliyobainishwa katika ripoti hii, ninaishauri Serikali ihakikishe:

(i) Hatua stahiki kuhakikisha kuwa miradi yote iliyokamilika inatumika kwa kikamilifu ili kufanikisha malengo yaliyokusudiwa na kupata thamani ya fedha. Pia, ichukue hatua madhubuti kuhakikisha miradi inayosuasua inakamilika kwa wakati.

(ii) Hatua za haraka kurejesha kiasi cha shilingi milioni 207.37 kilichotumika kulipa watumishi hewa.

(iii) Mamlaka za Serikali za Mitaa, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, pamoja na Ofisi ya Rais - Menejiment ya Utumishi wa Umma zinashirikiana na Hazina kuhakikisha kuwa fedha zinatengwa katika bajeti ili kulipa madai ya watumishi.

(iv) Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ujumla zinakuwa na mfumo wa kuhakikisha kwamba makato ya kisheria yanawasilishwa kwa Taasisi husika ili kuepuka matumizi yasiyo na tija yatokayo na riba.

(v) Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazingatia taratibu zilizowekwa ili kuhakikisha kwamba malipo yaliyolipwa yamepitishwa na Mamlaka sahihi katika ngazi zote ili kupunguza matumizi yasiyoridhisha ya fedha na kuisababishia Serikali hasara.

(vi) Mamlaka za Serikali za Mitaa zinaongeza juhudi katika urejeshaji wa fedha za mikopo ili kufanikisha malengo na uendelevu wa Mfuko wa Wanawake na Vijana. Pia, Mamlaka za Serikali za Mitaa zinashauriwa kuanzisha mikakati ya uhakika itakayochochea wakopaji kurejesha mikopo kwa hiari ili kusaidia ukuaji endelevu wa mfuko.

(vii) Mamlaka za Serikali za Mitaa zinatekeleza Kanuni ya 28(1) ya Kodi ya Mapato (vifaa vya mfumo wa kielektroniki) ya Mwaka 2012 kwa kufanya miamala na watoahuduma waliosajiliwa kwa kutumia mashine za stakabadhi za kielektroniki.

(viii) Kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa husika, inazingatia Sheria ya Manunuzi ya Umma pamoja na Kanuni zake. Pia, hatua stahiki zinachukuliwa dhidi ya wajumbe wote wa kamati za tathmini ya zabuni pamoja na wajumbe wa bodi za zabuni waliosababisha hasara.

(ix) Kupitia Mamlaka za Serikali za Mitaa husika, mikataba yote inayotekelezwa imewekewa dhamana kwa mujibu wa sheria na kanuni za manunuzi ili kulinda maslahi ya umma katika utekelezaji wa miradi.

(x) Mamlaka za Serikali za Mitaa zote zinawashindanisha wazabuni ili kupata bei shindani na bidhaa na huduma zenye ubora na thamani ya fedha.

## SURA YA TANO

## MATOKEO YA UKAGUZI WA MASHIRIKA YA UMMA

### 5.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa Mashirika ya Umma. Maeneo yaliyokaguliwa ni Mwenendo wa Kifedha na Uwezo wa Kuendelea kutoa Huduma; Usimamizi wa Mapato katika Mashirika ya Umma; Ongezeko la Madeni ya Wafanyakazi katika Taasisi za Elimu ya Juu; Ukamilishaji wa Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa; Hali ya Mali za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Ukusanyaji wa Madeni ya Wateja wa Mamlaka za Maji; na Usimamizi wa Mikataba na Manunuzi katika Mashirika ya Umma.

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Ukaguzi wa Mashirika ya Umma ulibaini masuala mbalimbali ambayo, Serikali inapaswa kuyafanyia kazi ili kuboresha usimamizi wa Rasilimali za Umma kama ifuatavyo.

### 5.2 Udhaifu katika Mwenendo wa Kifedha na Uwezo wa Kuendelea kutoa Huduma

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Katika ukaguzi wangu, nilibaini kuwepo kwa Mashirika ya Umma 14 yenye matatizo makubwa ya kifedha pamoja na kupata hasara hadi kusababisha madeni kuwa zaidi ya mitaji yao kwa zaidi ya asilimia 100. Aidha, kati ya Mashirika hayo, Mashirika 11 yana ukwasi hasi kwa maana yanajiendesha kwa hasara kwa zaidi ya miaka 2 sasa. Kufuatia hali hii, ni dhahiri kuwa Mashirika hayo hayawezi kujiendesha bila kutegemea msaada kutoka Serikali Kuu. Hivyo, ipo hatari ya kushindwa kuendelea kutoa huduma kwa jamii. Jedwali Na. 14 linaainisha Taasisi zenye hali mbaya kifedha.

**Jedwali Na. 14: Taasisi Zenye Hali Mbaya Kifedha**

| Na. | Taasisi | Na. | Taasisi |
|---|---|---|---|
| 1 | Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) | 8 | Baraza la Taifa la Bishara |
| 2 | Baraza la Michezo la Taifa | 9 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Mtwara |
| 3 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Lindi | 10 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Mwanza |
| 4 | Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) | 11 | Kampuni ya Usafirishaji na Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Usambazaji wa Umeme |
| 5 | Bodi ya Utalii Tanzania | 12 | Kampuni ya Simu (TTCL - Pesa) |
| 6 | Shirika la Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Dar es Salaam (DAWASCO) | 13 | Bodi ya Maziwa Tanzania |
| 7 | Kampuni ya Maendeleo ya Nishati ya Joto Tanzania (TGDC) | 14 | Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Dar es Salaam (DAWASA) |

## 5.3 Udhaifu wa Usimamizi wa Mapato katika Mashirika ya Umma

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Katika mapitio ya usimamizi wa mapato katika Mashirika ya Umma mbalimbali, nilibaini dosari zikiwemo;

### 5.3.1 Udhaifu katika ufuatiliaji wa marejesho ya kiasi cha shilingi trilioni 1.46 cha mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeshindwa kufahamu walipo wakopaji wa mikopo ya elimu ya juu yenye thamani ya shilingi trilioni 1.46. Kiasi hiki cha fedha ni kikubwa sana ikizingatiwa kuwa Kifungu cha 4(h) cha Sheria ya Bodi kinaitaka Bodi kutengeneza mtandao na kushirikiana na Taasisi na Mashirika mbalimbali ili kuwatambua wadaiwa na kuwezesha kupata marejesho ya mikopo hiyo.

### 5.3.2 Changamoto katika ukusanyaji wa tozo za maegesho ya meli

Mamlaka ya Mapato Tanzania inakusanya tozo za maegesho ya meli kwa niaba ya Mamlaka ya Bandari Tanzania na kila mwisho wa mwezi Mamlaka ya Bandari Tanzania inafanya uwianishaji wa kibenki. Hata hivyo, wakati wa ukaguzi wa mapato ya maegesho niligundua utofauti wa shilingi bilioni 42.5 katika kumbukumbu za Mamlaka ya Bandari Tanzania na zile za Mamlaka ya Mapato Tanzania. Hali hii inatokana na ukosefu wa ushirikiano wa kutosha kati ya Mamlaka hizi mbili katika uwianishaji wa taarifa pindi inapotokea tofauti.

### 5.2.1 Udhaifu wa utawala bora katika mashirika ya umma

Kwenye taarifa zangu za ukaguzi kwa miaka ya fedha 2015/16 na 2016/17 niliripoti kuwa Mashirika ya Umma 18 na 20, mtawalia, yalikuwa yakijiendesha bila kuwa na Bodi za Wakurugenzi kwa muda mrefu. Nilishauri Mamlaka za Uteuzi kuchukua hatua za makusudi kuteua Wakurugenzi ili kuboresha Utawala Bora na Udhibiti wa Ndani wa Taasisi husika. Katika ukaguzi wangu wa mwaka 2017/18 nimebaini kuwa Mashirika 24 hayakuwa na Bodi za Wakurugenzi. Kati ya Mashirika haya, saba (7) yanafanya kazi bila ya kuwa na bodi kwa zaidi ya mwaka mmoja, huku Mashirika manne (4) yakiwa na zaidi ya miaka miwili.

## 5.4 Ongezeko la Madeni ya Wafanyakazi katika Taasisi za Elimu ya Juu

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Kuanzia mwaka wa fedha 2016/17 hadi 2017/18, madeni yanayohusiana na malipo ya posho ya majukumu kwa wahadhiri wa Vyuo Vikuu vya Mzumbe na Ardhi yameongezeka. Katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, madeni yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1.49 hadi shilingi bilioni 3.41, na kwa Chuo Kikuu cha Ardhi, madeni yameongezeka kutoka shilingi bilioni 1.48 hadi bilioni 2.26. Aidha, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Mzumbe vilikuwa na madeni ya kiinua mgongo ya shilingi bilioni 5.59 na shilingi milioni 525, mtawalia kwa wafanyakazi ambao wamemaliza mikataba yao. Vilevile, Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine kilikuwa na madeni ya shilingi bilioni 6.78 ikiwa ni posho za nyumba na madeni

mengineyo ya wafanyakazi tangu Juni 2017. Hali hii inaweza kusababisha kushuka kwa kiwango cha elimu ya juu kutokana na wahadhiri kukosa morali ya kazi.

## 5.5 Ucheleweshaji wa Ukamilishaji wa Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Shirika la Nyumba la Taifa lilianzisha Mradi wa Nyumba wa Golden Premier Residence (711-2) uliopo Kawe, Kitalu Na. 711/2 mnamo tarehe 16 Oktoba, 2013. Katika mapitio yangu, nilibaini mradi huo ulisimama tangu mwanzo wa mwaka 2017 kutokana na ukosefu wa fedha. Hadi unasimama, mradi ulikuwa umekamilika kwa asilimia 30 na umetumia jumla ya shilingi bilioni 34.87, ambapo vyanzo vya ndani vilichangia kiasi cha shilingi bilioni 11.64 na mkopo kutoka Benki ya Uwekezaji Tanzania (TIB) ulikuwa ni shilingi bilioni 23.23.

Shirika la Nyumba la Taifa lilitakiwa kuanza kulipa marejesho ya Mkopo kuanzia Julai 2018. Hivyo, Shirika linatumia fedha kutoka vyanzo vingine kulipa mkopo huo huku mradi ukiwa haujakamilika. Ikiwa Shirika la Nyumba la Taifa halitapata kibali cha kukopa kutoka Wizara ya Fedha na Mipango kutokana na kufikia ukomo wake wa kukopa, litapaswa kuwalipa wakandarasi jumla ya shilingi bilioni 99.99 kwa kuvunja mikataba. Pia, litatakiwa kurejesha jumla ya shilingi bilioni 2.6 kwa wateja waliokwishaanza kulipia malipo ya awali ya ununuzi wa nyumba hizo.

## 5.6 Kupungua kwa Mali za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Japokuwa makusanyo ya mwaka yanaendelea kuwa makubwa zaidi ya malipo ya huduma za bima ya afya, kwa sasa malipo ya huduma za afya yanakua kwa uwiano mkubwa mwaka hadi mwaka zaidi ya uwiano wa kukua kwa mapato. Kutokana na hali hii, makisio ya madai ya huduma za bima ya afya pekee ifikapo mwaka wa fedha utakaoishia Juni 2024 yatakuwa ni asilimia 99.2 ya jumla ya makusanyo yote. Uwiano huu unakisiwa kuongezeka zaidi hadi kufikia asilimia 104.8 katika mwaka unaofuata.

Hali hii inamaanisha kwamba madai ya huduma za bima ya afya yanaendelea kuongezeka, na itafikia kipindi ambapo makusanyo na mapato kutoka katika uwekezaji hayataweza kukidhi madai na hivyo itaulazimu Mfuko kuchukua hatua za dharura kama kuuza mali zake.

## 5.7 Udhaifu katika Ukusanyaji wa Shilingi Bilioni 97.58 za Madeni ya Wateja wa Mamlaka za Maji

Nilibaini kuwepo kwa kiwango kidogo cha kukusanya marejesho ya madeni ndani ya Mamlaka za Maji, kwa kuwa mapato mengi yalikuwa hayajakusanywa na yamezidi muda uliowekwa kwenye Sera ya Mikopo ya Mamlaka husika. Katika jumla ya deni hilo la shilingi bilioni 97.58, nilibaini kuwa shilingi bilioni 39.59 (sawa na asilimia 41) ni Madeni ya Serikali, na shilingi bilioni 57.99 (sawa na asilimia 59) ni madeni ya wateja wengine. Ongezeko hili la madeni limesababishwa na ufuatiliaji hafifu wa wadeni na kutokufuata Sera ya Mamlaka za Maji ya kukata huduma za maji kwa wateja wanaokiuka taratibu.

## Udhaifu katika Usimamizi wa Mikataba na Manunuzi katika Mashirika ya Umma

Kampuni Hodhi ya Kusimamia Rasilimali za Shirika la Reli (RAHCO) ilifanya malipo ya awali ya kiasi cha Dola za Marekani 500,000 ikiwa ni sawa na shilingi bilioni 1.07 mwaka 2015 kwa mhandisi mshauri kwa kazi ya kutoa huduma ya ushauri ya ujenzi wa Reli ya Kisasa (Standard Gauge). Hata hivyo, huduma hiyo haikutolewa hadi kufikia Februari 2019, ikiwa ni miaka mitatu tangu malipo yalipofanyika. Mkataba ulikuwa wa miezi 12 kuanzia tarehe ya kusaini mkataba ambayo ilikuwa tarehe 20 Mei, 2015.

Aidha, Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS) kiliingia mkataba na Kampuni ya SUMSANG C & T Corporation tarehe 16 Desemba, 2014 kwa ajili ya kuleta na kufunga mfumo unaojulikana kama "OCS 121 System Viewer". Mfumo huu ulifungwa tarehe 26 Julai, 2017 kwa mkataba wa Dola za Marekani milioni 1.41. Hadi kufikia wakati wa ukaguzi, mfumo huo ulikuwa haujaanza kutumika kwa kuwa ulikuwa haujakidhi vigezo vilivyokuwa vimeainishwa kwenye mkataba.

## 5.8 Mapendekezo

*Ndugu Waandishi wa Habari,*

Ili kurekebisha kasoro zilizobainishwa katika ripoti hii, ninaishauri Serikali ihakikishe:

(i) Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu inashirikiana na Taasisi zingine na vyanzo vingine vya taarifa ili kuiongezea nguvu kanzidata yake na kuweza kuwatambua wakopaji ambao hawajulikani walipo.

(ii) Mamlaka ya Bandari Tanzania na Mamlaka ya Mapato Tanzania zinaboresha uwianishaji wa kibenki katika eneo la tozo za maegesho ya meli ili kuhakikisha unafanyika kwa ufanisi na usahihi na tofauti za kimahesabu zinamalizwa kwa wakati.

(iii) Inaangalia upya muda wa uhakiki wa madeni ya wafanyakazi kwani kuendelea kuchelewesha malipo hayo kunazidisha ongezeko la madai na hivyo kuongeza mzigo kwa Serikali.

(iv) Kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iangalie namna bora ya kuepusha hasara inayoweza kupatikana kutokana na kutokukamilika kwa mradi wa Nyumba wa Golden Premier Residence.

(v) Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS) kinafanya ufuatiliaji wa karibu ili mzabuni akamilishe vigezo vya mfumo ambavyo bado havijapatikana ili mfumo uanze kufanya kazi.

# SURA YA SITA

## MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO

### 6.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo. Maeneo yaliyohusika na Ukaguzi ni Kutorejeshwa kwa Fedha za Miradi zilizokopwa; Kodi ya Ongezeko la Thamani kulipwa kinyume na makubaliano ya Miradi; na Uchangiaji usioridhisha wa Serikali kwenye Miradi kinyume na makubaliano na Wadau wa Maendeleo. Maeneo mengine ya Ukaguzi ni Utekelezaji Hafifu wa Usambazaji wa Umeme Vijijini kupitia Mradi wa Wakala wa Nishati Vijijini; Kasi ndogo ya Utekelezaji wa Shughuli za Mradi wa Uboreshaji wa Makazi; Ucheleweshaji wa kukamilika kwa Ujenzi wa Miradi ya Maji; na kutotumika kwa Mradi wa Dampo uliokamilika.

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo umebaini masuala mbalimbali ambayo Serikali inapaswa kuyafanyia kazi ili kuboresha usimamizi wa rasilimali za umma. Masuala hayo yameainishwa kwa kina katika Ripoti ya Miradi ya Maendeleo, ambayo nimeiwasilisha kwako leo na muhtasari wake ni kama ifuatavyo;

### 6.2 Kutorejeshwa kwa Fedha za Mradi Shilingi Milioni 939.92 Zilizokopwa

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa Maofisa Masuuli wa miradi saba walikopa fedha za miradi jumla ya shilingi milioni 939.92 kwa ajili ya kugharimia matumizi ya kawaida kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Fedha hizi hazikurejeshwa kwenye miradi husika na hivyo kuathiri utekelezaji wa shughuli za miradi zilizopangwa.

### 6.3 Kodi ya Ongezeko la Thamani ya Shilingi Bilioni 12.16 Iliyolipwa Kinyume na Makubaliano ya Miradi

Ukaguzi wangu ulibaini kuwa malipo ya kodi ya ongezeko la thamani kiasi cha shilingi bilioni 12.16 yalifanywa na watekelezaji wa miradi 45 kinyume na makubaliano ya mikataba ya utekelezaji wa miradi husika.

### 6.4 Uchangiaji wa Serikali Usioridhisha kwenye Miradi kiasi cha Shilingi Bilioni 111.01 Kinyume na Makubaliano na Wadau wa Maendeleo

Ukaguzi wangu wa miradi mbalimbali kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018 ulibaini kuwa miradi kumi ambayo Serikali ilitakiwa kuchangia kiasi cha shilingi bilioni 118.44, ilichangia shilingi bilioni 7.43, sawa na asilimia sita tu. Hali hii ilisababisha upungufu wa kiasi cha shilingi bilioni 111.01 kinyume na makubaliano na wadau wa Maendeleo. Serikali kushindwa kuchangia miradi hii kwa kiasi kikubwa kumeathiri utekelezaji wa miradi husika na kudhoofisha juhudi za kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## 6.5 Utekelezaji Hafifu wa Wakala wa Nishati Vijijini Kusambaza Umeme Vijijini

Ukaguzi wa Miradi ya Nishati ulibaini kuwa Wakala wa Nishati Vijijini ilipanga kusambaza umeme kwenye vijiji vya Tanzania Bara vinavyokadiriwa kufikia 12,268 kuanzia mwaka 2013 hadi kufikia mwaka 2021. Hata hivyo, kufikia tarehe 30 Juni, 2018, mradi huo ulikuwa umefikisha umeme kwenye vijiji 4,395 tu, sawa na asilimia 36 kwa kipindi cha miaka mitano. Hali hii inaondoa uwezekano wa kufikia lengo la kusambaza umeme kwenye vijiji 7,873 vilivyobaki katika kipindi cha miaka mitatu iliyosalia hadi 2021.

## 6.6 Kasi Ndogo ya Utekelezaji wa Shughuli za Mradi wa Uboreshaji Makazi

Mradi wa uboreshaji wa makazi unatarajiwa kukamilika mnamo tarehe 28 Juni, 2019. Hata hivyo, ukaguzi ulibaini kuwepo kwa kiasi kikubwa cha fedha ambacho hakijatumika cha Dola za Marekani milioni 36.25 sawa na shilingi bilioni 81.80. Kiasi hiki ni sawa na asilimia 60 ya fedha za mkopo wa Dola za Marekani milioni 60 zilizotolewa kwa ajili ya mradi huu. Kuwepo kwa kiasi kikubwa cha fedha za mradi ambazo hazijatumika kumesababishwa na kasi ndogo ya utoaji wa mikopo na mchakato mrefu wa manunuzi. Hivyo, kuna uwezekano mdogo wa fedha hizi kutumika kufikia mwishoni mwa mwezi Juni 2019.

## 6.7 Kuchelewa Kukamilika kwa Ujenzi wa Miradi ya Maji

Ukaguzi wa miradi ya maji ulibaini kuwa miradi ya maji 65 inayotekelezwa na Halmashauri 22 za Mamlaka za Serikali za Mitaa yenye thamani ya shilingi bilioni 63.7 ilichelewa kukamilika kwa kipindi cha kati ya miezi 3 hadi 48. Uchelewaji huu ulitokana na uwepo wa wakandarasi wasio na

uwezo; ucheleweshaji wa fedha kutoka Serikalini, changamoto za usanifu wa michoro; na mapungufu yatokanayo na manunuzi.

## 6.8 Kutotumika kwa Mradi wa Dampo Uliokamilika Wenye Thamani ya Shilingi Bilioni 2.96

Ukaguzi wangu ulibaini uwepo wa Mradi wa Dampo wa thamani ya shilingi bilioni 2.96 mjini Kigoma Ujiji, ambao licha ya ujenzi wake kukamilika, Dampo hilo halikuwa limeanza kutumika. Hali hii ilitokana na Ujenzi wa Shule ya Msingi karibu na mradi huo na hivyo kutumika kwa dampo lile kunaweza kuleta athari za Kimazingira kwa Wanafunzi na Miundombinu ya Shule.

## 6.9 Mapendekezo

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Ili kurekebisha kasoro nilizozibainisha katika ripoti yangu, ninaishauri Serikali ihakikishe:

(i) Fedha zilizolipwa kama kodi ya ongezeko la thamani kwenye miradi 45 iliyosamehewa kodi zinarejeshwa ili kufanikisha utekelezaji wa shughuli za miradi ya maendeleo husika. Aidha, ninashauri watekelezaji wa miradi kuzingatia mikataba ya makubaliano na wadau wa miradi ya maendeleo kwa kuhakikisha kuwa miradi iliyosamehewa kodi hailipi kodi hizo ili kusaidia kukamilika kwa wakati miradi hiyo.

(ii) Inaweka utaratibu wa uwajibikaji ili kuhakikisha fedha za miradi zinapelekwa kwa wakati na kulingana na bajeti iliyoidhinishwa ili kutokuathiri utekelezaji kwa ufanisi wa miradi hiyo.

(iii) Inaanzisha ofisi itakayokuwa na jukumu la kuratibu utekelezaji wa miradi yote ya maendeleo nchini.

## SURA YA SABA

## MATOKEO YA UKAGUZI WA MIFUMO YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

### 7.1 Utangulizi

Sura hii inatoa muhtasari wa matokeo ya ukaguzi wa mifumo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA). Masuala yaliyobainika wakati wa ukaguzi ni pamoja na kuwepo kwa mgawanyo hafifu wa kazi ambazo hazitakiwi kufanywa na mtu mmoja kwenye mifumo; mifumo ya TEHAMA kutokuwa tangamani; Maofisa Masuuli kuidhinisha maombi ya malipo Nje ya Mfumo; na kutohakiki Bidhaa na Mizigo inayopita Nchini kwenda Nchi zingine kwenye Mfumo wa Pamoja wa Forodha (TANCIS). Masuala mengine yaliyobainika ni ufuatiliaji hafifu wa Makato ya asilimia moja (1.1%) kwa watoa huduma wa simu za mkononi kutoka kwenye Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki; Watumishi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) kutojengewa uwezo wa kusimamia Mfumo wa Usajili kupitia Mtandao; na Mifumo tofauti ya TEHAMA kufanya kazi moja.

***Ndugu Waandishi wa Habari***

Serikali kwa muda mrefu sasa imekua ikiwekeza katika mifumo ya TEHAMA ili kuongeza ufanisi katika shughuli zake zikiwamo ukusanyaji wa mapato na utoaji huduma kwa jamii. Kwa kutambua umuhimu wa mifumo hiyo na vihatarishi katika uunganishaji wa mifumo mipya, Ofisi yangu imejikita katika kuhakikisha ninakagua mifumo hiyo kwa umakini mkubwa na kutoa ripoti zitakazowezesha uboreshaji wa utendaji wa mifumo hiyo.

Katika mwaka wa fedha 2017/18, nimekagua mifumo mikubwa mitatu, ambayo ni Epicor kwa TAMISEMI; Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali-watu (HCMIS - Lawson) katika Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma; na Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki (GePG) katika Wizara ya Fedha na Mipango. Aidha, nimekagua mifumo ya udhibiti wa ndani ya TEHAMA kwa mashirika mbalimbali ya umma na wizara, pamoja na usimamizi wa miradi ya TEHAMA. Ukaguzi wangu ulibaini mapungufu yafuatayo.

## 7.2 Mgawanyo hafifu wa Kazi zisizotakiwa kufanywa na Mtu Mmoja kwenye Mifumo

### 7.2.1 Udhibiti hafifu katika mfumo wa Epicor katika Mamlaka za Serikali za mitaa

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Tathmini ya mfumo wa Epicor katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ilibaini kuwepo kwa mapungufu katika mgawanyo wa kazi zisizotakiwa kufanywa na mtu mmoja. Aidha, nilibaini kuwa watunza hazina wa Halmashauri mbalimbali walikuwa na uwezo wa kuingiza taarifa za bajeti, kufanya mgawanyo wa fedha, kuanzisha malipo, kuandaa hati za malipo, na kuidhinisha malipo hayo. Majukumu haya yakifanywa na mtu mmoja yanaweza kusababisha ubadhirifu wa fedha kwani mfumo wa udhibiti unakuwa dhaifu.

### 7.2.2 Udhibiti hafifu katika Mifumo ya Makusanyo ya Mapato ya Kiuhasibu katika Taasisi za Umma

Ukaguzi wangu ulibaini uwepo wa mifumo dhaifu ya Makusanyo ya Mapato ya Kiuhasibu katika Mashirika ya Umma. Mathalani, Mfumo wa Kiuhasibu katika Shirika la Viwango Tanzania (TBS) haujawekwa katika mazingira ya kumzuia mtumiaji kuidhinisha miamala ya kifedha, ambayo ameianzisha mwenyewe. Ukaguzi wangu ulibaini kuwa kati ya hati 44,280 za malipo ambazo zilitengenezwa kutoka kwenye mfumo wa malipo ya kielektroniki wa Shirika, hati 192 zilianzishwa, kuidhinishwa, na kuthibitishwa na mtu mmoja.

Vilevile, mapitio niliyoyafanya katika mfumo wa SURLIS wa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchikavu na Majini (SUMATRA) yalibaini kuwa hatua zote tatu za kutoa leseni zinafanywa na mtu mmoja, ambaye ana uwezo wa kuingiza taarifa za magari, kuthibitisha taarifa hizo, kuidhinisha, na kutoa hati za madai.

Hali-kadhalika, katika mapitio ya mfumo wa MIS pamoja na vyeti vya usajili wa bidhaa za chakula na dawa katika Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) nilibaini kuwa kati ya maombi 2,782 yaliyopokelewa, maombi 286 yalifanyiwa tahmini, kukaguliwa, na kuidhinishwa na mtu mmoja.

### 7.2.3 Udhaifu katika udhibiti wa Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki

Mapitio ya Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki yalibaini kuwa mtumiaji wa mfumo mwenye jukumu la umeneja ana uwezo wa kuweka tarehe ya ukomo wa malipo ya ankara bila kuidhinishwa hali inayopelekea mazingira ya udanganyifu. Aidha, nilibaini kuwa meneja anaweza kutengeneza ankara ya malipo na kupata namba ya kumbukumbu ya malipo kutoka kwenye mfumo. Pia, mfumo hauna hatua ya ziada ya kuidhinishwa kwa ankara hivyo inaweza kupelekea meneja kukadiria kiasi cha chini ikilinganishwa na kiwango halisi kinachotakiwa kulipwa.

## 7.3 Mifumo ya TEHAMA kutokuwa Tangamani

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Mapitio zaidi ya mifumo ya TEHAMA yalibaini kuwa mifumo hiyo haijaunganishwa na hivyo kuathiri utendaji wa pamoja wa shughuli za Serikali.

### 7.3.1 Kutounganishwa Mfumo wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, Epicor na TISS

Ukaguzi ulibaini kuwa Mfumo wa Epicor wa Mamlaka za Serikali za Mitaa hauna ushirikiano wa moja kwa moja na mfumo wa TISS, na hivyo kusababisha uwezekano kufanya malipo mara mbili.

### 7.3.2 Kutounganishwa Mfumo wa Epicor na Mfumo wa Akaunti Moja ya Hazina

Mfumo wa Epicor wa Mamlaka za Serikali za Mitaa haujaunganishwa na mfumo wa Akaunti Moja ya Hazina. Hivyo, katika mapitio ya uhamishaji wa fedha za Serikali za Mitaa kutoka benki za biashara kwenda Benki Kuu nimebaini mapungufu ya udhibiti katika kuhakikisha kuwa kiasi cha fedha kinachoonekana kwenye mfumo wa Epicor kinalingana na kiasi halisi cha fedha kilichotumwa kutoka benki za biashara kwenda Benki Kuu.

### 7.3.3 Kutokuunganishwa Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali-Watu (HCMIS - Lawson), "Ajira Portal", na Mfumo wa Epicor

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Ukaguzi wangu wa mifumo ya TEHAMA umebaini pia kuwa Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali-Watu (HCMIS - Lawson) haujaunganishwa na Mfumo wa Epicor, na “Ajira Portal”. Hali hii inaweka uwezekano wa kuwapo kwa wafanyakazi hewa katika mfumo wa HCMIS - Lawson. Mifumo hii mitatu ingekuwa imeunganishwa, ingeweza kuondoa uwezekano wa kuwapo wafanyakazi hewa kwa sababu mfumo wa “Ajira Portal” ulianzishwa ili kusimamia mchakato wa ajira kuanzia hatua ya maombi ya kazi, usaili, hadi uajiri. Mfumo huu una uwezo wa kutengeneza namba ya utambulisho ya kipekee kwa mtu anayeajiriwa ambayo inatumika kama namba ya mwajiriwa mpya kwenye mfumo wa HCMIS - Lawson. Vilevile, kutounganishwa kwa Mfumo wa Epicor na Mfumo wa HCMIS - Lawson kumepelekea kutengeneza bajeti ya rasilimali-watu nje ya mfumo wa HCMIS - Lawson. Hii inaweza kusababisha hatari ya kufanya matumizi ya Rasilimali-Watu zaidi ya bajeti iliyoidhinishwa.

### 7.3.4 Kutokuunganishwa kwa Mifumo ya Kiuhasibu “Accounting software” na Mifumo ya Makusanyo ya Mapato

Ukaguzi wa mifumo ulibaini kuwa Mfumo wa Kiuhasibu na mfumo wa makusanyo ya mapato haijaunganishwa. Ukaguzi ulibaini pia kuwa Mfumo wa Leseni na Maombi (LOIS) wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA); Mfumo wa Udhibiti wa Uchambuzi wa Usanifu wa Kiuhandisi (EDAMS) wa Mamlaka ya Maji Safi na Usafi wa Mazingira, Dar es Salaam (DAWASCO), na Mfumo wa Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani wa Mradi wa Mabasi ya Mwendokasi, Dar es Salaam (DART) haijaunganishwa na Mfumo wa Uhasibu. Hali hii inasababisha taarifa za mapato yaliyokusanywa na Taasisi hizi kuingizwa kwenye Mfumo wa Kiuhasibu na mtumiaji wa mfumo husika ambapo inaweza kupelekea kutokea kwa makosa ya kibinadamu na kusababisha kutowiana kwa taarifa zilizo kwenye mfumo wa mapato wa Taasisi na Mfumo wa Uhasibu.

### 7.3.5 Maofisa Masuuli Kuidhinisha Maombi ya Malipo Nje ya Mfumo

Mapitio ya Mifumo ya Kiuhasibu na Mifumo inayoendesha kazi za Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, na Mashirika ya Umma yameonesha kuwa Maofisa Masuuli wanaidhinisha nyaraka zilizochapishwa nje ya mfumo badala ya kuidhinisha kwenye nyaraka za ndani ya mfumo.

Hii imesababishwa na mifumo kutotengenezwa kwa namna inayowawezesha Maofisa Masuuli kuingia kwenye mfumo na kuidhinisha. Badala yake, maofisa wa chini huingiza taarifa kwenye mfumo ambazo zimeshaidhinishwa na Maofisa Masuuli kwenye nyaraka.

## 7.4 Bidhaa na Mizigo inayopita Nchini kwenda Nchi zingine kutohakikiwa kwenye Mfumo Jumuishi wa Forodha (TANCIS)

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Ukaguzi wangu ulibaini kuwa bidhaa na mizigo inayopita nchini kwenda nchi zingine hupita bila kuhakikiwa kwenye Mfumo wa TANCIS. Mapitio ya taarifa za TANCIS kuhusu bidhaa zinazosafirishwa kupitia mipaka ya Kabanga, Rusumo, Mutukula, Tunduma, na Kasumulu yalibaini kuwa miamala 599 ya bidhaa zilipita nchini kwenda nchi zingine pasipo kuhakikiwa kwenye mfumo wa TANCIS.

## 7.5 Ufuatiliaji hafifu wa Makato ya Asilimia 1.1 kutoka kwa Watoa huduma za Simu za Mkononi kutoka Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki

Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iliingia mkataba na watoa huduma za simu za mkononi kuwezesha mwingiliano wa Mfumo wa Serikali wa Malipo ya Kielektroniki kwa makato ya asilimia 1.1 ambayo itatozwa kwa kila malipo yanayofanywa na mteja. Kupitia ukaguzi wangu, nimebaini kuwa hakuna mfumo mzuri wa kuhakiki makato ya asilimia 1.1 kama yanatekelezwa. Ilibainika kuwa ukaguzi wa kushtukiza unafanyika mara mojamoja, ambapo ukaguzi huo si wa ufanisi na haujitoshelezi.

## 7.6 Watumishi wa Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) Kutokujengewa Uwezo wa Kusimamia Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao

Katika mapitio ya mradi wa BRELA wa Kubuni, Kuunda, Kusanidi, na Utekelezaji wa Mfumo wa Usajili kwa Njia ya Mtandao, nilibaini kuwa BRELA inamtegemea mkandarasi wa mfumo huo kutokana na kutokuwajengea uwezo wafanyakazi wake kusimamia na kuendesha mfumo huo baada ya kukabidhiwa. Hali hii inasababisha gharama kubwa za uendeshaji kwa BRELA.

## 7.7 Mifumo tofauti ya TEHAMA inayofanya Kazi Moja

Katika mapitio ya mifumo ya TEHAMA katika Taasisi mbalimbali za Serikali, nilibaini kuwepo kwa mifumo tofautitofauti inayofanya kazi moja. Jedwali Na. 15 linaonesha mifumo mbalimbali inayofanya kazi za aina moja.

**Jedwali Na. 15: Baadhi ya Mifumo ya TEHAMA Inayofanya Kazi Moja**

| Mfumo | Taasisi | Kazi ya Mfumo |
| --- | --- | --- |
| HCMIS - Lawson | Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | Kusimama na kuhakiki taarifa za mishahara ya wafanyakazi |
| GSPP | Wizara ya Fedha na Mipango | |
| National Business Portal | Wizara ya Viwanda, Uwekezaji, na Biashara; na BRELA | Usajili na utoaji wa leseni za biashara "Daraja B" |
| LGRCIS | Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa | |
| Salary Slip Portal | Wizara ya Fedha na Mipango | Kutoa hati za malipo ya mishahara |
| Watumishi Portal | Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora | |

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Kuwepo kwa mifumo katika Taasisi tofauti za Umma inayofanya kazi za aina moja kunasababisha kuwepo kwa gharama kubwa za uendeshaji kwa Serikali ambazo zingeokolewa kama kungekuwepo na uratibu wa utangamani wa mifumo ya Serikali na kazi zake.

## 7.8 Mapendekezo

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Kutokana na masuala yaliyobainishwa katika sura hii, ninaishauri Serikali ihakikishe:

(i) Taasisi za Serikali zinaimarisha udhibiti wa mifumo ya ndani pamoja na usalama wa taarifa za mifumo ya TEHAMA wakati wa utekelezaji wa mifumo hiyo.

(ii) Inaunda na kukiwezesha kitengo mahsusi cha uratibu na usimamizi wa miradi ya TEHAMA chini ya Wakala ya Serikali Mtandao (e-GA) ili kuratibu uanzishaji na utekelezaji wa mifumo ya TEHAMA katika Taasisi za Umma.

(iii) Kupitia Wakala ya Serikali Mtandao (e-GA), isimamie kikamilifu mifumo ya ankara ili kuhakikisha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato.

(iv) Maofisa Masuuli wanapatiwa uwezo wa kuingia na kuangalia miamala yote katika mifumo ya kiuhasibu na mapato; pamoja na kuweza kufanya marekebisho na marudio katika ankara za wateja ili waidhinishe kikamilifu kabla hazijatolewa.

## SURA YA NANE

## MATOKEO YA KAGUZI MAALUMU

### 8.1 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo ya ukaguzi maalumu uliofanywa na Ofisi yangu. Ukaguzi ulifanyika kuhusiana na Ununuzi wa Mfumo usiofanya kazi katika Shirika la Bima la Taifa; Malipo Hewa kwa Mzabuni yaliyofanywa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Udanganyifu katika Malipo ya shilingi milioni 267.89 kwenye Akaunti ya Matumizi Mengine katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo; na Malipo Hewa katika Kandarasi za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'. Maeneo mengine ambayo Ukaguzi Maalumu ulifanyika ni Ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) katika Jeshi la Polisi Tanzania; ujenzi wa Uwanja wa Ndege Songwe; na Ununuzi wa Sare za Askari Polisi uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania.

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Ofisi yangu ilifanikiwa kufanya kaguzi maalumu katika Taasisi mbalimbali za Umma. Yafuatayo ni baadhi ya mapungufu niliyoyabaini.

### 8.2 Shirika la Bima la Taifa kuwa na Mfumo usiofanya kazi ulionunuliwa kwa Gharama ya Dola za Marekani Milioni 3.59

Shirika la Bima la Taifa liliingia mkataba wa kununua mfumo wa 'Genisys' tarehe 18 Juni, 2012 kwa ajili ya kufungamanisha kazi kuu tatu za Shirika ambazo ni Bima ya Maisha, Bima zisizo za Maisha, na Uhasibu. Shirika liliukubali na kuupokea mfumo na kulipa Dola za Marekani milioni 3.59. Hata hivyo, ukaguzi wangu umebaini kuwa mfumo huo haufanyi kazi kikamilifu, hivyo kusababisha Shirika kutumia mfumo mwingine uitwao UNISYS. Kutokana na changamoto hizi, thamani ya fedha zilizotumika katika kununua mfumo huu haijaweza kupatikana kwani malengo ya kununuliwa kwake hayakufikiwa.

### 8.3 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kufanya Malipo Hewa ya Shilingi Bilioni 2.61 kwa Mzabuni

Katika uchunguzi wa vitabu vya fedha, taarifa za benki, na hati za malipo za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya nilibaini kuwepo kwa malipo ya kiasi

cha shilingi bilioni 3, kati ya malipo hayo shilingi bilioni 2.61 yalikuwa malipo hewa; shilingi milioni 350.87 ni malipo ambayo walipwaji walishindwa kubainika; na shilingi milioni 42.6 hazikuweza kuthibitika kupokelewa na walipwaji. Malipo haya yalitakiwa kulipwa watoa huduma za afya kwa kutumia hundi zilizofungwa lakini yalifanywa kwa fedha taslimu kinyume na Kanuni za Fedha za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

### 8.4 Udanganyifu katika Malipo ya Shilingi Milioni 267.89 kwenye Akaunti ya Matumizi Mengine katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Nilikagua malipo mbalimbali katika Akaunti ya Matumizi Mengine na nilibaini kuwa kwa nyakati tofauti kuna watumishi walianzisha, kupitisha, na kufanya malipo ya ya shilingi milioni 267.89 ambayo hayakuwa na viambatisho husika na mengine yalikuwa na viambatisho vyenye shaka.

### 8.5 Upotevu wa Mapato ya Zaidi ya Shilingi Bilioni 3.4 katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'

Mapitio ya mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani yalibaini mapungufu mbalimbali ikiwemo Halmashauri ya Wilaya ya Hanang kushindwa kuwasilisha vitabu 425 vya kukusanyia mapato. Mambo mengine yaliyobainika ni pamoja na:

(a) Upotevu wa mapato ya ndani ya Halmashauri ya jumla ya shilingi bilioni 1.04 yaliyokuwa yanakusanywa na mawakala; na

(b) Kutopatikana kwa nyaraka muhimu za makampuni ya mawakala wa ukusanyaji wa mapato kwa mikataba yenye thamani ya shilingi bilioni 2.36

### 8.6 Malipo Hewa ya Shilingi Milioni 73.45 katika Kandarasi za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji katika Halmashauri ya Wilaya ya Hanang'

Ukaguzi maalumu umebaini kuwa fedha kiasi cha shilingi milioni 73.45 za Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Maji zililipwa kwa wakandarasi kama dharura bila kuwepo kazi za dharura. Ukaguzi umebaini kutokuwepo kwa

ushahidi wowote wa kufanyika kwa kazi hiyo, na hivyo kudhihirika kuwa matumizi hayo ni hewa.

## 8.7 Ununuzi wa Mashine za Mfumo wa Kidigitali wa Usajili wa Wapiga kura (BVR) Uliofanywa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi

Nilibaini kuwa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ilinunua mashine za BVR 8,000 kwa ajili ya usajili wa wapiga kura, ambapo kati ya hizo, mashine 5,000 hazikukidhi vigezo vilivyoainishwa kwenye mkataba hivyo kusababisha kutolandana kimatumizi na vile vilivyonunuliwa hapo awali na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Wakala wa Taifa wa Usajili, Ufilisi, na Udhamini (RITA). Kutolandana huku kumeisababishia Serikali hasara ya shilingi milioni 862.08 zilizotumiwa na NIDA kununulia leseni mpya za “Windows” na “Biometric Algorithms” ili kubadilisha mashine 5,000 zilizopokelewa kutoka NEC ziweze kufanya kazi na mfumo wa BVR wa NIDA.

Aidha, nilibaini kuwa mzabuni alilipwa kiasi cha Dola za Marekani milioni 72.30 badala ya Dola milioni 72.15, kiasi ambacho kilikuwa bei ya mkataba hivyo kuwa na ongezeko la Dola za Marekani 148,243.73. Pia, mafunzo kwa maofisa 15 wa TEHAMA wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi hayakufanyika licha ya mzabuni kulipwa Dola za Marekani 358,650 kwa ajili ya mafunzo hayo.

## 8.8 Ununuzi wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) Uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Ukaguzi maalumu wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole (AFIS) ulibaini mambo yafuatayo:

(a) Mahitaji ya kitaalamu kutoka idara inayotumia mfumo huo hayakuzingatiwa wakati wa kutathmini na kutoa zabuni.

(b) Malipo ya shilingi bilioni 3.30 yalifanyika kwa mzabuni kwa ajili ya huduma ya matengenezo na msaada wa kitaalamu wa Mfumo wa Utambuzi wa Alama za Vidole kwenye mikoa nane ya Kipolisi ya Temeke, Mwanza, Simiyu, Rukwa, Tabora, Kigoma, Geita, na Kinondoni lakini Jeshi la Polisi lilishindwa kuthibitisha kuwa matengenezo hayo na msaada wa kitaalamu ulifanyika.

(c) Vifaa vya Utambuzi wa Alama za Vidole vyenye thamani ya shilingi bilioni 1.73 havikufungwa kwenye magereza 35 yaliyoainishwa. Badala yake vilihifadhiwa katika Ofisi ya Upelelezi, Makao Makuu ya Jeshi la Polisi.

(d) Malipo ya shilingi milioni 604.39 kwa ajili ya mafunzo kwa wataalamu 30 hayakufanyika.

(e) Jeshi la Polisi lilishindwa kuionesha timu yangu ya ukaguzi zilizo monita 58 za kompyuta aina ya Dell zenye thamani ya shilingi milioni 159.16 zilizopelekwa kwenye Kitengo cha Uchunguzi wa Kisayansi cha Makao Makuu ya Jeshi la Polisi (Forensic Unit). Pia, monita 213 za kompyuta aina ya Dell zililipiwa kiasi cha shilingi milioni 195.22 kwa mzabuni Lugumi Enterprises Limited lakini mzabuni hakuzileta.

## 8.9 Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Katika ukaguzi maalumu wa ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Songwe, Mbeya nilibaini mambo yafuatayo:

(a) Malipo ya jumla ya shilingi bilioni 1.43 yalifanyika mara mbili kwa udanganyifu kupitia maofisa wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege (TAA). Aidha, jumla ya shilingi bilioni 1.95 zililipwa bila ya kuwepo kwa jedwali la vipimo na hati za madai zilizoidhinishwa na mhandisi mshauri.

(b) Kati ya malipo ya awali ya shilingi bilioni 1.70 alizolipwa mkandarasi kwa ajili ya kuanza shughuli za ujenzi, ni shilingi milioni 176.56 tu ndizo zilizorejeshwa. Hivyo, bakaa ya shilingi bilioni 1.52 haikurejeshwa hadi ukaguzi huu unafanyika.

(c) Shilingi milioni 570.50 zililipwa zaidi ya gharama zilizoidhinishwa na mhandisi mshauri.

(d) Jumla ya shilingi bilioni 5.48 zililipwa kwa mkandarasi bila ya kuidhinishwa na mhandisi mshauri.

## 8.10 Ununuzi wa Sare za Askari Polisi Uliofanywa na Jeshi la Polisi Tanzania

Katika ukaguzi huu maalumu, nilibaini kuwa Jeshi la Polisi Tanzania lililipa jumla ya shilingi bilioni 16.66 bila ya kuwapo na ushahidi wa uagizaji na upokeaji wa Sare za Askari Polisi kwa Boharia Mkuu wa Jeshi la Polisi. Pia, nilibaini maoni ya Kisheria ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali yanayohusu uwasilishaji wa Kiapo cha Nguvu ya Kisheria (Power of Attorney) na leseni halali ya biashara hayakuzingatiwa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani wakati wa kusaini Mkataba Na. ME.014/PF/2015/2016/G/30 Lot 2 uliohusu ununuzi wa sare za askari polisi.

## 8.11 Mapendekezo

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

Kutokana na matokeo ya ukaguzi maalumu nilioufanya katika maeneo yaliyoelezwa, ninaishauri Serikali:

(i) Kuchukua hatua stahiki za kisheria na kinidhamu dhidi ya maofisa waliohusika katika ubadhilifu wa Mali za Umma. Pia, Mamlaka husika zihakikishe kuwa mianya yote niliyobainisha wakati wa ukaguzi inayopelekea upotevu wa Mali za Umma inazibwa.

(ii) Kupitia Shirika la Bima la Taifa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi, iwasiliane na wazabuni ili kuhakikisha kwamba masuala yote yaliyobaki kama ilivyooneshwa katika Hati za Mahitaji ya Kazi za Mifumo yanatatuliwa na kwamba mifumo hiyo inafanya kazi kikamilifu kama ilivyotarajiwa.

(iii) Kupitia Jeshi la Polisi Tanzania, ihakikishe kuwa vifaa vya Utambuzi wa Alama za Vidole vinafungwa katika maeneo husika na kuanza kutumika kama ilivyokusudiwa

## SURA YA TISA

### MATOKEO YA UKAGUZI WA UFANISI

### 9.1 Utangulizi

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Sura hii inawasilisha kwa Muhtasari Matokeo ya Ukaguzi wa Ufanisi. Matokeo haya yamegawanywa katika sehemu mbili, ambazo ni Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi, na Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi katika Sekta Mbalimbali. Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi inahusu Upatikanaji na Usambazaji Hafifu na Udhibiti Usioridhisha wa Pembejeo za Kilimo; Utoaji Usioridhisha wa Huduma za Ugani kwa Wakulima; Utoaji Hafifu wa Huduma Saidizi kwa Wasindikaji wa Mazao ya Kilimo; Usimamizi wa Milipuko ya Magonjwa na Visumbufu vya Mimea; na Usimamizi Usiojitosheleza wa Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji.

Kwa upande wa Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi katika Sekta Mbalimbali, Ukaguzi ulihusu Usimamizi wa Miradi ya Maji Vijijini; Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya za Rufaa na Dharura katika Hospitali za Rufaa za Ngazi ya Juu; Usimamizi wa Ujenzi wa Majengo Mijini; na Usimamizi wa Miradi ya Maji ya Visima Virefu. Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi katika Sekta Mbalimbali ulihusu pia Matengenezo ya Mitambo ya Kuzalisha Umeme; Ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Magari ya Serikali kwa Pamoja; Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu; na Usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Bima ya Afya zinazotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Katika ukaguzi wa ufanisi nimeandaa ripoti ya jumla na ripoti zingine 11 zinazogusa maeneo mbalimbali katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo nchini. Ripoti ya jumla imelenga uchambuzi wa masuala ya maendeleo ya sekta ya kilimo; wakati ripoti zingine zimelenga maeneo ya ukaguzi ambayo niliyapa kipaumbele katika mpango-kazi wa mwaka wa fedha 2017/18. Ufuatao ni muhtasari wa ripoti hizo:

### 9.2 Ripoti ya Jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi

*Ndugu Waandishi wa Habari,*
Yafuatayo ni baadhi ya masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa ufanisi kwenye sekta ya kilimo.

### 9.2.1 Upatikanaji na Usambazaji hafifu na Udhibiti usioridhisha wa Pembejeo za Kilimo

(a) Wizara ya Kilimo haitekelezi kiufanisi hatua za kutambua mahitaji halisi ya pembejeo za kilimo ili kuhakikisha upatikanaji wake kwa wakulima. Takwimu zinaonesha kuwa, kwa kipindi cha miaka 4 iliyopita, wastani wa usambazaji wa pembejeo za kilimo ulikuwa asilimia 39 tu ya mahitaji. Hii ilisababishwa na Wizara ya Kilimo kukadiria mahitaji ya pembejeo kwa kutumia taarifa za miaka iliyopita ambazo si za kuaminika.

(b) Mfumo wa usambazaji wa pembejeo za kilimo kwa wakulima haufanyi kazi vizuri katika kuhakikisha kuwa usambazaji unafanyika kwa wakati. Kulikuwa na ucheleweshaji wa pembejeo kwa kipindi cha kati ya miezi mitatu (3) hadi mitano (5) kwa pembejeo. Ucheleweshaji huu ulitokana na Wizara ya Kilimo kuchelewa kusambaza vocha za kununulia pembejeo.

(c) Ukaguzi ulibaini uwepo wa mbegu za mahindi ambazo hazikuwa na uwezo wa kuota, kwa mfano Pioneer 2859 na DKC 90-89. Pia, ukaguzi ulibaini uwepo wa zaidi ya asilimia 50 ya wauzaji wa pembejeo ambao hawakusajiliwa na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu vya Kitropiki, Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu, na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania; na wauzaji waliokuwa wanafanya biashara kinyume cha sheria kwa kutothibitishwa kufanya biashara; na wauzaji wa pembejeo wa msimu. Hali hii inasababisha usambazaji wa pembejeo kufanyika bila ya kufuata taratibu za usambazaji, kwa mfano uuzaji wa pembejeo katika masoko ya mnada badala ya kuuzwa katika maduka yaliyoidhinishwa.

(d) Wizara ya Kilimo pamoja na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu vya Kitropiki hazikufanya tathmini za kutosha za afya na mazingira ili kuhakikisha usalama wa viuatilifu vinavyosajiliwa. Tathmini za afya kwa wakulima zimekuwa zikifanyika kwa wakulima wakubwa tu na kuwaacha wakulima wadogo ambao wanakadiriwa kufikia asilimia

81 ya idadi ya Watanzania wote. Tathmini za mazingira zilizofanyika zimeonesha uwepo wa kiwango kikubwa cha DDT kwenye udongo zaidi ya kiwango kinachoruhusiwa kwa mujibu wa viwango vya kimazingira.

(e) Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu vya Kitropiki haikuweza kuhuisha mara kwa mara orodha ya viuwatilifu kama inavyotakiwa. Imebainika kuwa huwa inachukua kati ya miezi tisa (9) hadi miaka miwili (2) kuhuisha orodha ya viuwatilifu licha ya kuongezeka kwa kiwango cha matumizi.

(f) Kumekuwa na usajili hafifu wa mbolea na mbegu unaofanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania na Mamlaka ya Udhibiti wa Mbegu. Hali hii ilidhihirishwa na uwepo wa mbegu na mbolea zisizosajiliwa ambazo zilikuwa zinatumiwa na wakulima na kusababisha malalamiko ya ubora wa mbegu na mbolea hizo.

### 9.2.2 Utoaji usioridhisha wa Huduma za Ugani kwa Wakulima

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**

(a) Wizara ya Kilimo haikuandaa ipasavyo mipango ya utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima. Hali iliyosababisha kutowiana kwa rasilimali zilizokuwepo kwa ajili ya utoaji wa huduma za ugani kwa wakulima.

(b) Huduma za ugani hazikuweza kuwafikia wakulima kwa kiasi cha kutosha, ambapo ni asilimia 1 pekee ya wakulima walikuwa wamejiunga katika huduma ya mashamba darasa nchini. Pia, ni asilimia 17 tu ya vituo vya huduma za kilimo vya kata vilijengwa kwa ajili ya kutoa huduma kwa wakulima nchini.

(c) Wizara ya Kilimo haikuwajengea uwezo wa kutosha maofisa ugani ili kuwapa mbinu za kisasa katika kutoa huduma za ugani.

### 9.2.3 Utoaji hafifu wa Huduma saidizi kwa Wasindikaji kwa Mazao ya Kilimo

Wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati kama vile wasindikaji wa mazao ya kilimo hawakupatiwa huduma saidizi zinazojumuisha Mafunzo,

Fedha, Teknolojia, na Elimu ya Masoko. Takwimu zilionesha kuwa kwa miaka minne iliyopita Shirika la Maendeleo ya Viwanda Vidogo limeweza kutoa mafunzo kwa wajasiriamali na wenye viwanda vidogo na vya kati 60,888 ambao ni sawa na asilimia 0.4 ya makadirio ya idadi ya wajasiriamali nchini. Aidha, kwa kipindi cha miaka minne, Shirika lilipokea na kuthibitisha utoaji wa mikopo kwa maombi 35,315 lakini ilitoa mikopo kwa waombaji 22,563 sawa na asilimia 63 ya mikopo iliyothibitishwa.

### 9.2.4 Usimamizi wa Milipuko ya Magonjwa na Visumbufu vya Mimea

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

(a) Wizara ya Kilimo haikufanya vizuri majukumu yake ya usimamizi wa Milipuko ya Magonjwa na Visumbufu vya Mimea Nchini. Kumeonekana kuwa na kaguzi chache kwenye mipaka, na pia uelewa mdogo wa wakulima juu ya mbinu mbalimbali za kupambana na Milipuko ya Magonjwa na Visumbufu vya Mimea.

(b) Wizara ya Kilimo na TAMISEMI hazikudhibiti vya kutosha Milipuko ya Magonjwa na Visumbufu vya Mimea. Sababu mojawapo ni kutokuwepo kwa ufuatiliaji uliosaidia kutambua Magonjwa na Visumbufu vya Mimea; na

(c) Nilibaini kuwapo kwa uratibu duni kati ya Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Viuwatilifu vya Kitropiki na Kitengo cha Afya ya Mimea. Ofisi za Kitengo cha Afya ya Mimea zilizopo mipakani havikuwa na maabara zilizojitosheleza kufanya uchunguzi wa mizigo iliyoshikiliwa mipakani.

### 9.2.5 Usimamizi usiojitosheleza wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji

Katika ukaguzi wa ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji, nilibaini mapungufu yafuatayo:

(a) Upembuzi yakinifu haukufanyika kama ilivyopangwa ndani ya kipindi cha miaka minne (2014/15 hadi 2017/18). Taarifa zinaonesha kuwa mipango 11 tu ndiyo ilitekelezwa kati ya 360 sawa na asilimia 3. Upembuzi usio wa kina umepelekea kuacha baadhi ya vipengele ambavyo vimesababisha gharama za miradi kupanda kwa shilingi milioni 112.6.

(b) Kulikuwa na uchelewaji wa kukamilika kwa miradi ya umwagiliaji kwa asilimia 76 nje ya muda wa mkataba. Ilibainika kuwa kukosekana kwa mipango-kazi mahususi ya ujenzi ilikuwa ni sababu kuu ya miradi mingi kuchelewa kukamilika.

## 9.3 Ripoti za Ukaguzi wa Ufanisi katika Sekta Mbalimbali

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Yafuatayo ni baadhi ya masuala yaliyobainika katika ukaguzi wa ufaniki wa sekta mbalimbali.

### 9.3.1 Ukaguzi wa Usimamizi wa Miradi ya Maji Vijijini

Ukaguzi wa Usimamizi wa Miradi ya Maji Vijijini ulilenga kuangalia kiwango ambacho Wizara ya Maji na Ofisi ya Rais - TAMISEMI zinahakikisha upatikanaji wa Maji Safi Vijijini. Yafuatayo ni baadhi ya mapungufu yaliyojitokeza katika ukaguzi wangu:

(a) Miundombinu ya maji iliyojengwa vijijini ina uwezo wa kusambaza maji kwa asilimia 85.2 ya mahitaji ya watu vijijini wakati kiasi cha watu wanaopata maji ni asilimia 58.7 tu kutokana na baadhi ya miradi iliyojengwa kutofanya kazi.

(b) Asilimia 79 ya miradi 58 iliyokaguliwa haikukamilika kwa wakati kwa sababu mbalimbali ikiwemo ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi, uwezo mdogo wa kifedha na kiufundi wa wakandarasi, na usimamizi duni wa Wizara ya Maji na Mamlaka za Serikali za Mitaa husika.

(c) Theluthi moja (1/3) ya miradi ya maji iliyotekelezwa katika mikoa sita niliyotembelea ilikuwa na ongezeko la gharama kwa kati ya shilingi bilioni 1.2 na shilingi bilioni 7.1. Hii ilisababishwa na udhaifu katika usanifu wa michoro ya miradi, udhaifu katika uandaaji wa nukuu za ukubwa wa kazi, na uchambuzi hafifu wa mahitaji ya miradi husika.

### 9.3.2 Ukaguzi wa usimamizi wa Utoaji wa Huduma za Afya za Rufaa na Dharura katika Hospitali za Rufaa za Ngazi ya Juu

*Ndugu Waandishi wa Habari,*
Ukaguzi huu ulikuwa na lengo la kuangalia iwapo Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto ina mfumo madhubuti wa kuhakikisha ufanisi wa usimamizi wa utoaji Huduma za Afya za Rufaa na Dharura katika Hospitali za Rufaa na Ngazi za Juu. Mapungufu yaliyobainika ni kama yafuatayo.

(a) Idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa katika Hospitali za Rufaa na Ngazi za Juu inazidi uwezo wa hospitali husika kutokana na kupandishwa daraja kutoka Hospitali zinazotoa huduma za afya ya msingi kwenda daraja la juu pasipo kuzingatia miundombinu iliyopo, pamoja na idadi ya wagonjwa wanaohudumiwa katika hospitali hizo na upatikanaji wa madaktari bingwa.

(b) Huduma za Afya za Rufaa zitolewazo katika Hospitali za Rufaa Ngazi ya Juu hazijitoshelezi. Ingawa Wizara ya Afya haijaanzisha kiwango stahiki cha muda ambao wagonjwa wanapaswa kusubiri kabla ya kupata huduma ya afya, ukaguzi umebaini kuwa baadhi ya wagonjwa wenye rufaa na dharura husubiri kwa wastani wa saa 3 hadi 4 kabla ya kupata huduma.

*(c)* Hospitali sita (6) kati ya saba (7) za Rufaa za Mkoa nilizokagua hazikuwa zikitoa huduma zote za afya kama inavyostahili kutolewa na Hospitali ya Rufaa ikiwa ni pamoja na tiba za Magonjwa ya Kawaida, Huduma za Afya ya Watoto, huduma za Uzazi na Ujauzito, huduma za Kinywa na Meno, na huduma za Upasuaji.

(d) Wizara ya Afya haijafuatilia na kutathmini utendaji wa Hospitali za Rufaa katika utoaji wa Huduma za Afya za Rufaa na Dharura. Hii imesababishwa na kutokuwepo kwa mipango ya ufuatiliaji na kuainisha viashiria katika kufuatilia utendaji wa Hospitali za Rufaa.

### 9.3.3 Ukaguzi wa usimamizi wa Ujenzi wa Majengo Mijini

*Ndugu Waandishi wa Habari,*
Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini endapo ofisi ya Rais- TAMISEMI, kupitia Mamlaka ya Serikali za Mitaa inafuatilia kikamilifu shughuli za

ujenzi wa majengo mijini ili kuhakikisha majengo yote yanayojengwa yanazingatia viwango vinavyotakiwa na kwamba ni salama kwa matumizi. Yafuatayo ni baadhi ya mambo yaliyobainika wakati wa ukaguzi huu.

(a) Kuwepo kwa majengo katika maeneo yasiyopangwa na makazi yasiyo rasmi. Maeneo hayo yamekuwa na nyumba zenye ubora hafifu, zilizojengwa bila uwepo wa upatikanaji wa huduma muhimu kama vile barabara, mitaro ya maji ya mvua, huduma za maji safi, pamoja na huduma zingine za dharura.

(b) Kulikuwa na uchelewashaji wa vibali vya ujenzi kati ya mwezi mmoja hadi miaka miwili kuanzia pale maombi yalipowasilishwa na kibali kinapoidhinishwa. Mamlaka za serikali za mitaa hazikuwa na mifumo ya usajili wa maombi ya vibali vya ujenzi pamoja na utoaji wa elimu kwa umma juu ya mchakato na umuhimu wa vibali vya ujenzi.

(c) Mamlaka za serikali za mitaa hazikuwa na mikakati, mipango, miongozo mahususi ya ukaguzi wa shughuli za ujenzi wa majengo na bajeti za kufuatilia shughuli za majengo katika maeneo yao. Hapakuwa na kanzidata inayoonesha idadi na taarifa za majengo yanayoendelea kujengwa au kukamilika.

(d) Hakuna mawasiliano ya kueleweka kati ya taasisi muhimu kama vile Wakala wa Majengo Tanzania; Jeshi la Zimamoto na Uokoaji; Mamlaka za Serikali za Mitaa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi katika kupanga na kutekeleza shughuli za ujenzi wa nyumba mijini.

### 9.3.4 Ukaguzi wa usimamizi wa Miradi ya Maji ya Visima Virefu

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Maji inasimamia kwa ufanisi Miradi ya Maji ya Visima Virefu. Mapungufu yafuatayo yalibainika katika ukaguzi.

(a) Kati ya visima 1485 vilivyochimbwa, visima 490 sawa na asilimia 33 havikutoa maji. Jumla ya shilingi milioni 764 zilitumika katika miradi ya maji ya visima virefu ambavyo havikutoa maji.

(b) Jumla ya sampuli 709 kati ya 6,615 za maji zilizofanyiwa uchunguzi hazikukidhi viwango vya ubora kwa matumizi ya binadamu. Kulikuwa na viashiria vikubwa vya kutokuwepo kwa ubora wa maji kama vile uwepo wa kiwango kikubwa cha mangenisi, floridi, alkali, uchafu, na vimelea vya magonjwa. Hii imetokana na kutokuwepo kwa utafiti wa kutosha wa maji ya ardhini kwa nchi nzima.

(c) Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nane nilizotembelea, miradi ilichelewa kwa asilimia 50 wakati mradi mmoja ulichelewa kwa asilimia 78 ya muda wa ujenzi uliokadiriwa. Hali hii ilitokana na uwezo mdogo wa kiufundi na kifedha wa wakandarasi, kuchelewa kwa fedha za miradi kutoka Serikalini, na ucheleweshaji wa malipo kwa wakandarasi.

### 9.3.5 Ukaguzi wa matengenezo ya Mitambo ya kuzalisha Umeme

***Ndugu Waandishi wa Habari,***

Katika Ukaguzi wa matengenezo ya Mitambo ya kuzalisha Umeme inayosimamiwa na TANESCO, nilibaini maswala yafuatayo:

(a) Kuwepo kwa utafiti hafifu kuhusu bei halisi za vipuri vya mitambo yake. Hali hii ilisababisha baadhi ya vipuri kuwa juu ya bajeti kwa kiwango cha hadi asilimia 99 wakati baadhi ya vipuri vilikuwa na bajeti pungufu kwa kiwango cha hadi asilimia 116.

(b) Kutokuwepo kwa wataalamu maalumu na watengenezaji wa mitambo walioidhinishwa kufanya matengenezo. Hivyo, TANESCO inategemea wataalamu kutoka nje ya nchi kufanya matengenezo ya mitambo yake. Mapungufu haya yalionekana zaidi katika mitambo ya kuzalisha umeme wa gesi. TANESCO ilishindwa kupeleka wafanyakazi wake kujifunza kutoka kwa watengenezaji wa mitambo ili kupata ujuzi mahsusi.

(c) Kutofanyika kwa matengenezo yanayozingatia viashiria hatarishi ili kuweka vipaumbele katika udhibiti wa viashiria hivyo. Hali hii inaweza kusababisha nchi kukosa umeme wa uhakika na kushindwa kufikia malengo katika sekta mbalimbali za kiuchumi.

### 9.3.6 Ukaguzi wa ufanisi wa Mfumo wa Ununuzi wa Magari ya Serikali kwa Pamoja

***Ndugu Waandishi wa Habari*,**
Lengo kuu la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo Mfumo wa Ununuzi wa Magari ya Serikali kwa Pamoja unafanya kazi kwa kuzingatia gharama, muda, idadi, na viwango vya ubora wa magari. Mapungufu yafuatayo yalibainika.

(a) Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini (GPSA) haukuendesha ushindani madhubuti katika kufanya manunuzi ya magari ya Serikali.

(b) Bei iliyotolewa na Kampuni ya Toyota Tanzania ilikuwa juu kwa asilimia 15 hadi 49 ikilinganishwa na bei za magari za Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa kwa aina ya magari na viwango vya ubora vinavyofanana. Ilibainika kuwa Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini ukinunua magari ya viwango vya ubora vinavyofanana kutoka kwa mawakala wengine tofauti na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa, hupoteza takribani shilingi milioni 10 hadi 50 kwa kila gari moja lililonunuliwa.

(c) Ukaguzi ulibaini kuwa magari yaliyonunuliwa hayakufika kwa wakati wala kwa idadi iliyotakiwa. Ucheleweshaji wa magari ulikuwa kwa hadi siku 130.

(d) Taasisi nunuzi ziliwasilisha mahitaji yao ya magari kwa Wakala wa Huduma za Ununuzi Serikalini kwa wakati. Hata hivyo, Wakala umekuwa ukiagiza magari kulingana na mahitaji yaliyoletwa na taasisi nunuzi mojamoja badala kukusanya maombi hayo na kufanya manunuzi kwa pamoja jambo linaloiongezea Serikali gharama.

### 9.3.7 Ukaguzi wa usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi wenye Mahitaji Maalumu

*Ndugu Waandishi wa Habari*,

(a) Kuna upungufu wa asilimia 68 wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia ikiwemo mashine za kurudufisha na kuchapisha maandishi ya nuktanundu, shime-sikio, vifaa vya kupima kiwango cha usikivu na visaidizi kwa wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia, kuona, na ulemavu wa akili.

(b) Kuna upungufu wa walimu wa elimu maalumu kwa ngazi ya shule ya msingi kwa takribani asilimia 44. Walimu wa elimu maalumu waliopo ni 2460 kati ya walimu 4428 wanaohitajika nchini.

(c) Kwa kipindi cha miaka minne iliyopita, walimu 952 kati ya 2460 sawa na asilimia 39 ya walimu wa elimu maalumu hawakupatiwa mafunzo ya muda mfupi.

(d) Wizara ya Elimu haijaandaa utaratibu wa namna ambayo wanafunzi wenye ulemavu wa kuona watafanya mitihani ya hesabu na sayansi, kinyume na Kanuni Na. 29(3) ya Kanuni za Mitihani za Mwaka 2016.

### 9.3.8 Ukaguzi wa usimamizi wa Utoaji wa huduma za Bima ya Afya zinazotolewa na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya

*Ndugu Waandishi wa Habari*,

Lengo la ukaguzi lilikuwa ni kutathmini iwapo Wizara ya Afya, na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya unatekeleza kikamilifu majukumu yao ya usimamizi wa utoaji wa huduma za bima ya afya nchini. Mapungufu yafuatayo yalibainika.

(a) Hadi kufikia mwezi Juni 2018, ni asilimia 32 tu ya Watanzania ndiyo walikuwa wanatumia bima ya afya. Idadi hii inajumuisha wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii ambao ni asilimia 25 na wanachama wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya.

(b) Kumekuwepo na matumizi yaliyozidi kiwango cha uchangiaji wa wanachama katika makundi mbalimbali ya wanachama wa Mfuko. Kwa mfano, kundi la KIKOA, matumizi yalikuwa asilimia 710; kundi la viongozi wa dini, matumizi yalikuwa asilimia 401; kundi la Toto Afya

Kadi, matumizi yalikuwa asilimia 298; kundi la madaktari wa mafunzo kwa vitendo, matumizi yalikuwa asilimia 174; kundi la wanafunzi, matumizi yalikuwa asilimia 171; na kundi la wachangiaji binafsi, matumizi yalikuwa asilimia 160. Hali hii isipodhibitiwa, itadhohofisha hali ya kifedha na utendaji wa Mfuko.

(c) Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulitoa mkopo wa shilingi bilioni 24.6 kwa Wizara ya Mambo ya Ndani mwezi Agosti 2010 kwa ajili ya ununuzi wa magari ambapo wizara ilitakiwa kuanza kurejesha mkopo huo baada ya kipindi cha mwaka mmoja yaani Agosti 2011, kwa kipindi cha miaka nane. Hadi kipindi cha ukaguzi huu, mkopo huo ulikuwa bado haujarejeshwa.

(d) Mwaka 2012, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya ulitoa kiasi cha shilingi bilioni 114.1 kwa ajili ya kugharamia ujenzi wa Hospitali ya Benjamini Mkapa bila ya kuwa na makubaliano yoyote ya kimaandishi hali iliyosababisha kutolipwa kiasi chochote hadi kipindi cha ukaguzi huu.

## HITIMISHO

***Ndugu Waandishi wa Habari,***
Haya ni baadhi tu ya mambo ambayo yameainishwa katika ripoti zangu. Ni imani yangu kuwa mtapata muda wa kuyasoma kwa undani zaidi katika ripoti zangu ili muweze kuuelimisha umma pasipo kubadili maudhui ya taarifa zilizopo ndani ya ripoti hizo.

Aidha, ripoti hizi zinapatikana katika tovuti ya ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ambayo ni www.nao.go.tz pamoja na tovuti ya serikali yaani www.tanzania.go.tz. Pia, nakala laini zimeandaliwa kwa ajili ya kurahisisha kuuhabarisha umma.

Pia, natumia nafasi hii kumshukuru Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mh. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa ushirikiano wake na kipaumbele alichokitoa wakati wa kupokea ripoti hizi pamoja na serikali nzima ya awamu ya tano kwa namna ambavyo imekuwa ikiyafanyia kazi mapendekezo yangu. Ninalishukuru pia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na kamati zake za kudumu hususani PAC na LAAC kwa kendelea kutumia ripoti hizi katika kutekeleza majukumu yao.

Kwa namna ya pekee ninawashukuru waandishi wa habari kwa kuendelea kuhakikisha kuwa maswala yaliyoainishwa katika ripoti hizi yanaifikia jamii kwa wakati.

Prof. Mussa Juma Assad,
**Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali**
**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.**
**8 Aprili, 2019**